SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

# HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA RAIS - FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

**DKT: SAADA MKUYA SALUM**
**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS - FEDHA NA MIPANGO**

**JUNI, 2022**

# YALIYOMO


A. UTANGULIZI.......................................................................... 1
B. MAJUKUMU MAKUU YA OFISI YA RAIS - FEDHA NA MIPANGO ............................................................................. 2
C. MAFUNGU YA BAJETI YA OFISI YA RAIS - FEDHA NA MIPANGO.............................................................................3
D. UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA RAIS - FEDHA NA MIPANGO KWA KIPINDI CHA JULAI 2021 – MACHI 2022. ... 4
a) Mapato ya Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango .................................. 4
E. UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA PROGRAMU ZINAZOSIMAMIWA NA FUNGU F01 ............................................. 7
PF0101 – Programu kuu ya Bajeti na Usimamizi wa Fedha za Umma. 7
SF010101- Program Ndogo ya Usimamizi wa Hazina......................... 7
SF010102-Program Ndogo ya Usimamizi wa Bajeti ya Serikali .......... 8
SF010103-Programu Ndogo ya Uratibu wa Fedha za Nje .................... 9
SF010104 -Programu Ndogo ya Usimamizi wa Hesabu za Ndani........ 12
SF010105 - Programu Ndogo ya usimamizi wa Sekta ya Fedha na Sera za Kodi ............................................................................................ 13
SF010106- Program Ndogo ya Usimamizi wa Mifumo ya Udhibiti wa Fedha za Umma............................................................................. 14
PF0102 - Programu Kuu ya Usimamizi na Uwekezaji wa Mali za Umma.......................................................................................... 14
SF010201- Programu Ndogo ya Usimamizi wa Mitaji ya Umma......... 15
SF010202 - Programu Ndogo ya Usimamizi wa Ununuzi na Uhakiki wa Mali za Serikali ............................................................................ 15
PF0103 - Programu Kuu ya Uendeshaji wa Uratibu wa Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango.............................................................................. 16
SF010301 - Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji wa Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango – Unguja ................................................... 17
SF010302- Programu Ndogo ya Mipango Sera na Utafiti wa Sekta ya Fedha. ........................................................................................ 17
SF010303 - Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara -Pemba ................................................................... 18
F. UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA FUNGU F02...................... 19

G. UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA FUNGU F03 .................... 20
PF0301 - Programu Kuu ya kuratibu Mipango ya Kitaifa na Maendeleo ya Watendakazi .................... 21
SF030101 – Program Ndogo ya Uratibu wa Mipango ya Kitaifa na Kupunguza Umasikini .................... 21
SF030102 - Programu Ndogo ya Maendeleo ya Watendakazi na Masuala ya Idadi ya Watu. .................... 22
SF030103 - Programu Ndogo ya Ufuatiliaji na Tathmini wa Mipango wa Maendeleo. .................... 23
PF0302 -Programu Kuu ya Usimamizi wa Uchumi Mkuu, Tafiti na Takwimu .................... 24
SF030201 - Programu Ndogo ya Ukuzaji wa Uchumi. .................... 24
SF030202 - Programu Ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Shughuli za Takwimu Zanzibar. .................... 25
SF030203- Programu Ndogo ya Uratibu wa Tafiti na Ubunifu. .................... 26
PF0303 - Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Tume ya Mipango .................... 28
SF030301 - Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Mipango .................... 28
SF030302- Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa shughuli za Tume ya Mipango Pemba. .................... 29
H. UTEKELEZAJI WA MIRADI YA OFISI YA RAIS, FEDHA NA MIPANGO .................... 29
i. Mradi wa Mageuzi ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP-V) . 29
ii. Mradi wa Uimarishaji Rasilimali za ndani na Usimamizi wa Mali asili (ISP - DRMNRG). .................... 30
iii. Mradi wa Uimarishaji Utawala Bora (ISPGG III). .................... 31
iv. Ujenzi wa Ofisi za Serikali. .................... 31
v. Mradi wa Ukuzaji Uchumi Jumuishi BIG –Z. .................... 31
vi. Mradi wa Mpango wa Kuimarisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA). .................... 32
vii. Mradi wa Uendelezaji Takwimu Zanzibar (ZSDP). .................... 33
I. UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA TAASISI ZA OFISI YA RAIS FEDHA NA MIPANGO JULAI 2021 - MACHI 2022. .................... 34

a) Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB). ........ 34
b) Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ........ 35
c) Mfuko wa Barabara Zanzibar (ZRF) ........ 35
d) Mamlaka ya Manunuzi na Uondoaji wa Mali za Umma (ZPPDA) . 36
e) Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) ........ 38
f) Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) ........ 39
g) Shirika la Bima Zanzibar (ZIC) ........ 39
J. MWELEKEO WA BAJETI YA OFISI YA RAIS, FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA 2022-2023 ........ 40
Vipaumbele vya Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango ........ 40
Makadirio ya Mapato ya Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango ........ 42
PF0101- Programu Kuu ya Usimamizi wa Bajeti na Fedha za Umma.. 42
PF0102 – Programu Kuu ya Usimamizi na Uwekezaji wa Mali za Umma ........ 43
PF010104- Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango ........ 43
PF0201 – Programu Kuu ya Usimamizi wa Mfuko Mkuu wa Serikali. 43
PF0301 - Programu Kuu ya Uratibu wa Mipango ya Kitaifa na Maendeleo ya Watendakazi ........ 44
PF0302 - Programu Kuu ya Usimamizi wa Uchumi Mkuu na Utafiti... 44
PF0303 - Programu kuu ya Uendeshaji na Utumishi wa Tume ya Mipango ........ 44
PF0401- Programu Kuu ya Kuendeleza na Kuratibu Takwimu Rasmi za Kiuchumi na Kijamii ........ 45
PF0402- Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ........ 45
PF0501- Programu Kuu ya Usimamizi wa Hazina ........ 46
PF0502- Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Mhasibu Mkuu ........ 46
PF0601- Programu Kuu ya Usimamizi wa Ukaguzi wa ndani Serikalini ........ 46
PF0602 - Programu Kuu ya Utawala na Uendeshaji ........ 47
K. MIRADI YA MAENDELEO ITAKAYOSIMAMIWA NA OFISI YA RAIS, FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA 2022/2023 ........ 47

L. MWELEKEO WA BAJETI KWA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA WIZARA 2022/2023 .......... 49
M. SHUKRANI .......... 57
N.HITIMISHO .......... 58

## A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** Awali ya yote, naomba nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa Rehma zake kutujaalia neema ya uhai na afya na kuendelea kuwepo kwa amani na utulivu katika nchi yetu. Uwepo wa mambo yote haya yametuwezesha kukutana na kuniwezesha kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kuwasilisha Bajeti ya Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

2. **Mheshimiwa Spika,** Kwa heshima, naomba kuchukua fursa hii kipekee kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa imani yake kwangu kuendelea kunikabidhi majukumu ya kuitumikia Serikali hii ya Awamu ya Nane.

3. **Mheshimiwa Spika,** Naomba kutoa shukran maalum kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutoa mashirikiano kwa Rais wetu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Dkt. Hussein Ali Mwinyi hasa wakati nchi yetu ilipokumbwa na athari kubwa za kiuchumi na kijamii kutokana na maradhi ya Uviko -19 yaliyoanza mwaka 2019. Mashirikiano hayo yameiwezesha nchi kupata fedha Dola za Kimarekani 571 milioni sawa na takriban TZS 1.3 trilioni kutoka Shirika la Fedha Duniani (IMF) kwa ajili ya kutekeleza miradi na shughuli za kimaendeleo ili kukabiliana na athari zilizotokana na maradhi ya Uviko -19. Kati ya fedha hizo, Zanzibar imepatiwa Dola za Kimarekani 100 milioni sawa na TZS 230 bilioni ambazo zinatumika kuhuisha shughuli za kiuchumi na kijamii hapa nchini.

4. **Mheshimiwa Spika,** Napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza Wasaidizi Wakuu wa Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Othman Masoud Othman Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar na Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdullah Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, kwa kumshauri vyema Mhe. Rais wa Zanzibar na

Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na kuendelea kusimamia vyema majukumu yao ambayo ni chachu kwa maendeleo ya nchi yetu.

5. **Mheshimiwa Spika,** Nakupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Spika, Zubeir Ali Maulid kwa umakini na umahiri wako wa kuliongoza vizuri Baraza hili tukufu pamoja na Naibu Spika, Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma pamoja na Wenyeviti na Wajumbe wote wa Kamati za Baraza la Wawakilishi kwa kusimamia vyema shughuli za Baraza, kuendelea kutoa ushirikiano na kutushauri katika kutekeleza majukumu yetu.

6. **Mheshimwa Spika,** Baada ya maelezo ya utangulizi kwa ruhusa yako na kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 ilivyoelekeza ndani ya kifungu cha 88 kifungu kidogo (b) naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu likae na kujadili mapendekezo ya makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

## B. MAJUKUMU MAKUU YA OFISI YA RAIS FEDHA NA MIPANGO

7. **Mheshimiwa Spika,** Kimsingi, majukumu makuu ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango ni pamoja na haya yafuatayo:
   i. Kusimamia ukusanyaji wa mapato ya Serikali kutokana na vyanzo mbali mbali. Mapato hayo yanajumuisha mapato ya kodi na yasiyokuwa ya kodi, misaada na mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na Taasisi za Kifedha pamoja na mikopo ya ndani ikiwemo ile ya Hati Fungani;
   ii. Kusimamia mali za Serikali kupitia usimamizi wa ununuzi, utunzaji na uondoaji wa mali za Serikali pamoja na Hisa za Serikali katika Mashirika na Kampuni binafsi ambazo Serikali inamiliki;
   iii. Kusimamia Fedha za Umma na Shughuli za Uhasibu na Ukaguzi Serikalini. Katika jukumu hili Ofisi inasimamia Bajeti

ya Serikali, Usimamizi wa Hazina, Huduma za Uhasibu na Ukaguzi wa Ndani Serikalini;

iv. Kusimamia Deni la Taifa na kufuatilia mwenendo wa Deni la Taifa (Mikopo ya Ndani na Nje) na udhibiti wake;

v. Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa sera thabiti, mahiri na shirikishi za kodi na fedha;

vi. Ofisi inasimamia maendeleo ya Sekta ya Fedha, inayohusisha masuala ya Benki, Bima, Hifadhi ya Jamii na usimamizi wa Taasisi za Huduma Ndogo Ndogo za Fedha;

vii. Kusimamia Mifumo ya Ukusanyaji na Udhibiti wa Fedha za Umma;

viii. Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa na kuitafsiri kwenye mipango ya kipindi cha muda wa kati kwa kuzingatia idadi ya watu na mahitaji yake;

ix. Kuratibu na kusimamia maendeleo ya uchumi kupitia sekta za kiuchumi na kijamii;

x. Kuratibu Sera za Kisekta na kupunguza umasikini nchini;

xi. Kusimamia upatikanaji na utoaji wa takwimu rasmi kwa maendeleo ya nchi; na

xii. Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa mipango ya kitaifa na kimataifa.

## C. MAFUNGU YA BAJETI YA OFISI YA RAIS- FEDHA NA MIPANGO

**8. Mheshimiwa Spika,** Majukumu ya Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango, yanatekelezwa kupitia mafungu makuu sita (6) ambayo ni Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango (F01), Mfuko Mkuu wa Serikali (F02), Tume ya Mipango (F03), Mtakwimu Mkuu wa Serikali (F04), Mhasibu Mkuu wa Serikali (F05) na Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Hesabu za Serikali (F06).

## D. UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA RAIS- FEDHA NA MIPANGO KWA KIPINDI CHA JULAI 2021 – MACHI 2022

9. **Mheshimiwa Spika,** Kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha utekelezaji wa Bajeti kwa kipindi cha miezi tisa Julai – Machi 2021/2022 kama ifuatavyo:

### a) Mapato yaliyopangwa kukusanywa na Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango

10. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa mapato, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022, Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango kupitia Taasisi zake imepangiwa kukusanya jumla ya **TZS 1.783 Trilioni** ambapo mapato hayo yalijumuisha:

   i. TZS 525.1 bilioni zilizokadiriwa kukusanywa na Bodi ya Mapato Zanzibar;
   ii. TZS 413.1 bilioni zilizokadiriwa kukusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania;
   iii. TZS 283.1 bilioni zilizokadiriwa kupatikana kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kwa njia ya Mikopo na Misaada kwa miradi ya maendeleo;
   iv. TZS 20 bilioni zilikadiriwa kupatikana kwa mfumo wa Misaada ya Kibajeti kutoka kwa Washirika wa Maendeleo;
   v. TZS 220 bilioni Mikopo kutoka Taasisi za Fedha za Ndani na Nje kwa ajili ya miradi ya maendeleo;
   vi. TZS 122.34 bilioni za Mapato yasiokuwa ya kodi;
   vii. TZS 21 bilioni za mapato ya wafanyakazi wa Taasisi za Muungano wanaofanya kazi hapa Zanzibar;
   viii. TZS 92 bilioni mikopo ya ndani kwa njia ya hati fungani; na
   ix. Mapato mengineyo yasiyokuwa ya kodi 87.35 bilioni.

11. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha miezi tisa Julai 2021- Machi 2022, Ofisi imefanikiwa kukusanya TZS 836.289 bilioni sawa na asilimia 47 ya makadirio ya mwaka ya **TZS 1.783 Trilioni.** Hii ni

sawa na asilimia 80 ya kukusanya **TZS 1.05 trilioni** ndani ya kipindi cha Julai 2021-Machi 2022. Uchambuzi wa ukusanyaji na upatikanaji wa mapato hayo ni kama ifuatavyo:

i. **Mapato ya kodi,** Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) imekusanya TZS 275.179 bilioni sawa na asilimia 52 ya makadirio ya TZS 525.10 bilioni kwa mwaka na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) imekusanya TZS 256.362 bilioni sawa na asilimia 62 ya makadirio ya TZS 413.06 bilioni kwa mwaka;

ii. **Mapato yasiokuwa ya kodi** ya TZS 57.569 bilioni yamekusanywa sawa na asilimia 47 ya makadirio ya TZS 122.34 bilioni kwa mwaka;

iii. **Fedha zilizopatikana kutoka kwa Washirika wa Maendeleo** ni TZS 119.500 bilioni sawa na asilimia 42 ya makadirio ya TZS 283.09 bilioni kwa mwaka ikiwemo mikopo ya TZS 82.47 bilioni na misaada ya TZS 37.03 bilioni;

iv. TZS 2.348 bilioni zimepatikana sawa na asilimia 12 ya makadirio TZS 20 bilioni ya mwaka kama Misaada ya Kibajeti;

v. **Mapato mengineyo yasiyokuwa ya kodi** TZS 14.297 bilioni sawa na asilimia 16 ya makadirio ya TZS 87.35 bilioni;

vi. **Mapato yaliyopatikana kutokana na Kodi ya mapato ya wafanyakazi wa SMT wanaofanya kazi hapa Zanzibar** TZS 11.034 bilioni sawa na asilimia 53 ya makadirio ya TZS 21 bilioni; na

vii. **Mikopo ya ndani kupitia Hati Fungani iliyopatikana ni** TZS 100 bilioni sawa na asilimia 109 ya makadirio TZS 92 bilioni kwa mwaka.

Mchanganuo wa mapato unaonekana katika **Kiambatisho Namba 1.**

**b) Matumizi ya Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango**

**12. Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa matumizi Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango iliidhinishiwa kutumia TZS 402.15 bilioni kwa mafungu makuu matatu (3) ambayo ni Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango (F01);

Mfuko Mkuu wa Serikali (F02) na Tume ya Mipango (F03). Hadi kufikia Machi, 2022 fedha zilizopatikana na kutumika kwa mafungu hayo ni TZS 225.06 bilioni sawa na asilimia 56 ya makadirio ya TZS 402.15 bilioni ya mwaka. Kati ya fedha hizo, TZS 79.48 bilioni zilitumika kwa fungu (F01), TZS 136.95 bilioni zilitumika kwa fungu (F02) na TZS 9.00 bilioni zilitumika kwa fungu (F03).

13. **Mheshimiwa Spika,** Mchanganuo wa matumizi ya F01 (Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango) ni kama ifuatavyo:
    i. Mshahara TZS 7.38 bilioni;
    ii. Ruzuku kwa Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango TZS 17.43 bilioni;
    iii. Matumizi mengineyo (OC) TZS 14.46 bilioni; na
    iv. Matumizi ya kazi za maendeleo TZS 40.13 bilioni.

14. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa matumizi ya F02 (Mfuko Mkuu wa Serikali) mchanganuo wake ni kama ifuatavyo:
    i. Kulipa Mafao ya Kiinua Mgongo kwa kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022 jumla ya TZS 28.23 bilioni zimelipwa kwa wastaafu 1,753 kuanzia Januari 2021 hadi machi 2022 na pencheni jumla ya TZS 23.48 bilioni kwa wastaafu wastani wa 14,707 kwa mwezi;
    ii. Kulipa Riba na Mikopo jumla ya TZS 28.30 bilioni; na
    iii. Matumizi mengine ya Serikali kupitia Mfuko Mkuu ni TZS 56.94 bilioni.

15. **Mheshimiwa Spika**, Aidha, Mchanganuo wa matumizi ya F03 (Tume ya Mipango) ni kama ifuatavyo:
    i. Mshahara TZS 1.08 bilioni;
    ii. Ruzuku ya Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali TZS 1.42 bilioni;
    iii. Matumizi mengineyo (OC) TZS 680.00 milioni; na
    iv. Matumizi ya kazi za maendeleo TZS 5.82 bilioni.

    Mchanganuo wa matumizi kiprogramu unaonekana katika **Kiambatisho Namba 2.**

## E. UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA PROGRAMU ZINAZOSIMAMIWA NA FUNGU F01 (Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango)

**PF0101-Programu Kuu ya Bajeti na Usimamizi wa Fedha za Umma**

16. **Mheshimiwa Spika,** Lengo kuu la Programu hii ni kuimarisha usimamizi wa mapato na matumizi ya Serikali. Programu hii ilitarajiwa kutumia TZS 65.05 bilioni kutekeleza programu ndogo sita (6) zifuatazo:

**SF010101- Programu Ndogo ya Usimamizi wa Hazina**

17. **Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo ya Usimamizi wa Hazina ilikadiriwa kutumia TZS 35.01 bilioni kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Hadi Machi 2022, TZS 19.97 bilioni sawa na asilimia 57 ya makadirio ya mwaka zimepatikana na zimetumika kwa kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kusimamia ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Serikali yasiyokuwa ya kodi ambapo jumla ya TZS 130.93 bilioni zimeweza kukusanywa hadi Machi 2022;
ii. Kuandaa vikao vya ukomo wa matumizi ya Serikali kwa ajili ya kupanga na kuidhinisha matumizi ya Serikali kwa kila mwezi (Ceiling Committee Meetings); ambapo hadi Machi 2022, vikao tisa (9) vimefanyika kati ya vikao kumi na moja (11);
iii. Kuhudhuria kikao cha usuluhishi wa madeni ya nje baina ya Zanzibar na Tanzania Bara ambapo usuluhishi wa madeni hayo umefanyika; Taarifa za kina za madeni kwa upande wa Zanzibar zimeweza kupatikana na kutolewa katika nyakati tofauti na kurahisisha kujua Deni la Taifa kwa upande wa Zanzibar; na
iv. Kupatiwa mafunzo ya IPSAS na CPA watendaji 25 Unguja na Pemba kwa lengo la kuwawezesha kufunga mahesabu kwa viwango vya Kimataifa. Watendaji hawa wapo katika Taasisi mbali mbali

za Serikali na kwa sasa, taarifa za ufungaji wa hesabu zimekuwa zinatolewa kwa viwango vya kuridhisha ukilinganisha na kipindi cha awali.

**SF010102-Programu Ndogo ya Usimamizi wa Bajeti ya Serikali**

18. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo hii ina jukumu la kutayarisha Bajeti ya Serikali na kusimamia utekelezaji wake. Hadi Machi 2022, programu hii imetumia jumla ya TZS 10.45 bilioni sawa na asilimia 45 ya makadirio ya mwaka ya TZS 23.10 bilioni.

19. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo hii imejumuisha kifungu kidogo cha marekebisho ya mishahara ya makadirio TZS 21.67 bilioni. Hadi kufikia Machi 2022, kifungu hichi kimetumia TZS 10.03 bilioni.

20. **Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo ya Usimamizi wa Bajeti ya Serikali imetekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kufuatilia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha robo, nusu na mwaka. Ripoti tatu (3) zimetolewa kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2021/2022 pamoja na Ripoti ya Utekelezaji wa Bajeti kwa kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai 2021 hadi Machi, 2022;
ii. Kuratibu shughuli za uwekaji wa "GFS Code" kwa mfumo wa (Zan Malipo) pamoja na mfumo wa Bajeti na Matumizi (BAMAS) kwa Wizara na Taasisi zote za Serikali;
iii. Kuendesha majukwaa mawili ya Uchumi na Bajeti na kukusanya maoni kutoka Serikali Kuu na kutoka kwa wadau mbali mbali kwa ajili ya maandalizi ya bajeti ya mwaka 2022/2023. Maoni pamoja na ushauri ulitolewa na wadau wa majukwaa haya, yamezingatiwa katika Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2022/2023;
iv. Kushiriki vikao vitano (5) vya pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania vinavyohusiana na ukomo wa matumizi

pamoja na kikao cha ufuatiliaji wa mikopo ya hati fungani ambapo vimetuwezesha kujua rasilimali fedha zilizopatikana na mgao wa fedha unaokuja Zanzibar.

v. Kushajiisha uandaaji wa mpango wa matumizi kwa robo mwaka (quartely cash flow) na kutayarisha kibali cha matumizi kwa Serikali kuu kwa ajili ya utolewaji wa fedha na matumizi;

vi. Kukamilisha Rasimu ya Sheria ya Bajeti (Budget Act) ambapo rasimu ya awali imekamilika na shughuli zinazohusiana na matayarisho zimepangwa kuendelea kwa mwaka 2022/2023;

vii. Kuratibu uendeshaji wa warsha za kujenga uwezo wa watendaji na wadau wa Bajeti kwa mashirikiano ya IMF (kupitia East AFRITAC). Warsha hizo zimeweza kuwapatia watendaji uzoefu wa utayarishaji wa bajeti na utekelezaji wake; na

viii. Kuandaa na kukamilisha matayarisho ya Bajeti ya Serikali kwa hatua za awali kwa kuwakutanisha watendaji wakuu wa sekta na watendaji wa wizara na kujadili mipango ya mwaka wa fedha 2022/2023.

**SF010103-Programu Ndogo ya Uratibu wa Fedha za Nje**

**21.** **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo hii ina lengo la kuimarisha ufuatiliaji na upatikanaji wa misaada na mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Hadi Machi 2022, programu hii imetumia TZS 195.45 milioni sawa na asilimia 38 ya makadirio ya TZS 511 milioni kwa ajili ya kutekelezaji shughuli zifuatazo:

i. Kufuatilia fedha za Mkopo Euro 460 milioni kutoka Mfuko wa Fedha wa Kuhamasisha Biashara wa Uingereza kwa ajili ya miradi mipya ya miundo mbinu ya barabara zenye urefu wa kilomita 103.5. Barabara hizo ni ya Tunguu –Makunduchi (48 km), Fumba Kisauni (12 km), Mkoani – Chake chake (43.5 km) pamoja na Ujenzi wa uwanja wa Ndege wa Pemba. Majadiliano ya upatikanaji wa fedha za mkopo huu yanaendelea kupitia Kamati ya Madeni ya Kitaifa (NDMC) ya Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania;

ii. Vikao vitano (5) vimeratibiwa kwa ajili ya mapitio ya Rasimu ya

Mfuko wa Mabadiliko ya Tabia Nchi kwa wadau wa Serikali za Mitaa na Asasi za Kiraia Unguja na Pemba. Mikutano kama hii inasaidia kujua hali ya miradi ya kudhibiti athari za mabadiliko ya tabia nchi katika sehemu mbali mbali na kupanga mipango bora ya utafutaji wa rasilimali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kudhibiti athari za mabadiliko ya tabia nchi pamoja na kujenga uwezo wa wataalamu katika usimamizi wake.

iii. Kushiriki mkutano wa kitaifa wa Mradi wa Mazao ya Viungo utakaoimarisha maendeleo ya mnyororo wa thamani. Utekelezaji wa Mradi huu ni ikiwemo ujenzi wa Ghala la Kuhifadhia Mboga Mboga (Cold room) katika eneo la Sokoni Darajani pamoja na vizimba kumi (10) kwa ajili ya Wafanyabiashara wa mboga mboga;

iv. Kufuatilia fedha za mkopo Dola za Kimarekani milioni hamsini (USD 50 milioni) kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) wenye lengo la kutekeleza Mradi wa kuwawezesha vijana kujiajiri katika Uchumi wa Buluu chini ya usimamizi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Kupitia mradi huu, Serikali inakusudia kujenga Vyuo vya Amali, kukarabati na kutanua maeneo ya vyuo vya ufundi vilivyopo kikiwemo Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Karume; Hatua iliyofikiwa kwa sasa ni kuandaliwa kwa nyaraka ya tathmini ya mradi (Project Appraisal Document);

v. Kuratibu kwa upande wa Zanzibar; uwekaji saini wa makubaliano ya Mkopo kutoka Benki ya Dunia wa Dola za Kimarekani Milioni Tisa laki nne (USD 9.4 Milioni) kwa ajili ya mradi wa kikanda wa kuboresha Takwimu utakaoimarisha uwezo wa Wafanyakazi wa Takwimu ikiwemo ujenzi wa Ofisi za Mtakwimu Mkuu wa Serikali kwa upande wa Pemba; utengenezaji wa Mpango Mkuu wa Takwimu pamoja na kusaidia programu ya Sensa Tanzania na Zanzibar; Mradi huu unatarajiwa kuanza utekelezaji wake mwaka wa fedha 2022/2023;

vi. Kufuatilia upatikanaji wa fedha za mkopo nafuu Dola za

Kimarekani milioni 20 kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa Kuendeleza Afya ya Mama na Mtoto. Matarajio ya utekelezaji wa mradi huu utaanza mwaka wa fedha 2022/2023;

vii. Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa ombi la fedha Dola za Kimarekani 18.9 milioni kutoka Benki ya Korea Kusini kwa ajili ya maendeleo ya mradi wa Umwagiliaji maji kwenye bonde la Cheju B mradi ambao ni muendelezo wa mradi wa awali;

viii. Kuratibu na kufuatilia upatikanaji wa fedha kutoka Shirika la Maendeleo la Korea Kusini (KOICA) Dola za Kimarekani milioni tano na laki tano (USD 5.5 million) kwa ajili ya kutekeleza mradi wa kuwainua wanawake katika kilimo cha mazao ya baharini Zanzibar;

ix. Mafunzo 45 ya muda mfupi yameratibiwa na tisa 9 ya muda mrefu kwa watumishi wa Serikali kupitia Shirika la Maendeleo la Korea (KOICA) ambapo hatua inayoendelea ni kutathmini taarifa za watumishi na watakaobahatika wataanza mafunzo hayo;

x. Kuratibu maandalizi ya utekelezaji wa mradi wa Maendeleo ya kilimo na uvuvi unaofadhiliwa na shirika la Maendelo ya Kilimo Duniani (IFAD), wenye lengo la kusaidia sekta ya uvuvi na kilimo cha mazao ya baharini, ujenzi wa kiwanda cha samaki na ununuzi wa boti za uvuvi, ambapo Zanzibar imetengewa dola za kimarekani 8.8 milioni hatua inayofuata ni uzinduzi na kuanza rasmi kwa mradi;

xi. Kuratibu mikutano mitatu (3) ya majadiliano na Taasisi Zisizo za Kiserikali ikiwa na lengo la upatikanaji wa taarifa za misaada inayokuja Zanzibar kwa lengo la kusaidia huduma za jamii. Taarifa hizi zinaongeza ufahamu juu ya hali halisi ya mashirikiano ya Zanzibar na Washirika wa Maendeleo kupitia Asasi Zisizo za Kiserikali.

**SF010104 -Programu Ndogo ya Usimamizi wa Hesabu za Ndani**

22. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo hii ina lengo la kuimarisha usimamizi wa matumizi ya fedha za Serikali. Hadi Machi 2022, Programu ndogo hii imetumia jumla ya TZS I.57 bilioni sawa na asilimia 79 ya makadirio ya TZS 1.99 bilioni kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kukamilisha na kuchapisha Miongozo mitatu (3) ambayo ni; Muongozo wa Ukaguzi wa Ndani, Muongozo wa Uthibitisho wa Ubora na Muongozo wa Mpango Mkakati. Wakaguzi wa Hesabu za Ndani thamanini na tatu (83) walipatiwa mafunzo ya miongozo hiyo kwa ajili ya kuwasaidia katika kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi;

ii. Kupatiwa mafunzo ya stashahada ya IPSAS Wakaguzi ishirini na tano (25) wa Wizara na Taasisi za Serikali yaliyotolewa na Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi Tanzania ikiwa na lengo la kujenga uwezo kwa wakaguzi wetu katika ukaguzi wa hesabu kwa kutumia mfumo wa IPSAS;

iii. Kaguzi nne (4) maalumu katika Taasisi mbali mbali zikiwemo, ukaguzi wa mapato ya visa, ukaguzi wa mapato na matumizi ya Skuli ya Faraja, ukaguzi wa madeni ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ na ukaguzi wa madeni Mamlaka ya Maji Zanzibar.Taarifa ya kaguzi hizi zimewasilishwa kwa mamlaka husika kwa ajili ya hatua stahiki; na

iv. Kukamilisha zoezi la uhakiki wafanyakazi wa wizara, Idara na Taasisi zote za Serikali. Lengo la uhakiki huu ni kupata takwimu halisi ya wafanyakazi katika sekta ya umma, taarifa za ajira zao, kubaini wafanyakazi hewa pamoja na kufahamu kiwango halisi cha fedha za umma zinazotumika kwa wafanyakazi wa umma. Taarifa ya zoezi hili imekamilika na imewasilishwa kwa mamlaka husika kwa hatua stahiki.

**SF010105 - Programu Ndogo ya Usimamizi wa Sekta ya Fedha na Sera za Kodi**

23. **Mheshimiwa Spika,** Lengo la programu ndogo hii ni kuwa na sekta ya fedha iliyo imara itakayosaidia kukuza uchumi. Hadi Machi 2022, TZS 252.95 milioni zimepatikana na zimetumika sawa na asilimia 17 ya makadirio ya TZS 1.55 bilioni kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kupitia sheria tano (5), kanuni mbili (2) na muongozo mmoja (1) wa ukusanyaji wa mapato ya kodi na yasiyokuwa ya kodi. Kazi hiyo imeleta ufanisi wa kusimamia na kukusanya mapato ya Serikali pamoja na kuleta unafuu kwa wananchi;

ii. Kutolewa elimu kwa wajasiriamali mia moja na hamsini (150) Unguja na Pemba kuhusu umuhimu wa sekta ya fedha nchini na uelewa wa masuala ya fedha.Wajasiriamali wamepata uelewa katika biashara zao juu ya namna ya kufunga mahesabu, mwenendo wa biashara zao katika uwekaji wa kumbukumbu na uhifadhi wa fedha katika taasisi za fedha;

iii. Kushiriki kongamano la wiki ya elimu ya fedha na kufanya utafiti wa huduma za uwakala wa benki ili kutatua changamoto zinazowakabili Mawakala wanaotumia huduma za kibenki Tanzania;

iv. Kusimamia marekebisho ya Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu na Mapato Yatokanayo na Uhalifu nambari 10 ya mwaka 2009 ambayo imewasilishwa na kupitishwa Baraza la Wawakilishi mwezi wa Machi 2022;

v. Kupitia na kuchambua maombi yasiyopungua 223 ya misamaha ya kodi na kumshauri Mheshimiwa Waziri wa Nchi-Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango kuchukua hatua stahiki. Misamaha yenye thamani ya TZS 25.4 bilioni imetolewa kwa kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022 ikiwa ni sawa na punguzo la asilimia 63 ikilinganishwa na misamaha iliyotolewa katika kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ya TZS 69.9 bilioni;

vi. Kuundwa na kuanza kazi kwa Kamati Maalum ya Kufuatilia na Kutathmini Matumizi ya Misamaha ya Kodi inayotolewa na Serikali katika miradi na uwekezaji; ambapo kamati hiyo imeshaanza kazi rasmi na kwa hatua ya awali Kamati imeandaa ripoti itakayowasilishwa kwa hatua za utekelezaji;

vii. Kushiriki mikutano 31 ya kitaifa, kikanda na kimataifa inayohusiana na kodi, sekta ya fedha na masuala ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia. Hii imesaidia kujenga uwezo wa maafisa wa Idara inayosimamia sera za kodi na fedha. Rasimu ya Wazo la Awali la kuanzisha muundo na mfumo wa *Sovereign Wealth Fund* imekamilika.

viii. Kuanza maandalizi ya awali kwa ajili ya kazi za kuanzisha Soko la Hisa la Zanzibar. Tayari baadhi ya wataalamu katika Idara ya Sera za Kodi na Fedha wameshapata mafunzo ya awali katika Soko la Hisa la Dar-es-Salaam.

**SF010106- Programu Ndogo ya Usimamizi wa Mifumo ya Udhibiti wa Fedha za Umma**

**24. Mheshimiwa Spika,** Lengo la programu hii ni kuwa na mfumo bora wa kusimamia Mali za Umma. Hadi Machi 2022, programu ndogo hii imetumia TZS 363.98 milioni sawa na asilimia 13 ya makadirio ya TZS 2.88 bilioni. Fedha hizo zimetumika kwa manunuzi ya vifaa vya Tehama (ICT) vya Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango ambavyo vinasaidia katika ufanisi na utendaji kazi za usimamizi na udhibiti.

**PF0102 – Programu Kuu ya Usimamizi na Uwekezaji wa Mali za Umma**

**25. Mheshimiwa spika,** Lengo la programu hii ni kuwa na mfumo bora wa kusimamia mali za umma na uwekezaji wake. Hadi Machi 2022, programu hii imetumia TZS 35.25 bilioni sawa na asilimia 42 ya makadirio ya TZS 83.81 bilioni kwa ajili ya kutekeleza programu ndogo mbili zifuatazo:

**SF010201- Programu Ndogo ya Usimamizi wa Mitaji ya Umma**

**26.** **Mheshimiwa spika,** Lengo la programu ndogo hii ni kusimamia Mitaji ya Umma (zikiwemo majengo ya Serikali, vifaa na hisa za Serikali katika makampuni) ili kuhakikisha inakwenda sambamba na mabadiliko ya kiuchumi hapa Zanzibar na duniani katika kuleta tija na manufaa kwa umma. Hadi Machi 2022, TZS 35.19 bilioni zimetumika sawa na asilimia 42 ya makadirio ya TZS 83.59 bilioni kwa kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kuratibu ukamilishwaji ujenzi wa jengo la Mahakama Kuu ya Zanzibar lililopo Tunguu na kuendeleza ujenzi wa Jengo la Ofisi SMIDA lililopo Maruhubi;

ii. Kufanya tathmini ya mitaji na kuchambua hesabu za mashirika ili kupima utendaji na kuainisha faida iliyotengenezwa na mashirika hayo. Kufuatia tathmini hizo, Serikali imeweza kukusanya gawio la jumla ya TZS 5.8 bilioni kutoka Mashirika ya Serikali yenye kujiendesha kibiashara yakiwemo Benki ya Watu Zanzibar, Shirika la Bima Zanzibar, Shirika la Bandari Zanzibar na Shirika la Umeme Zanzibar;

iii. Kusimamia Mapato jumla ya TZS 436.34 milioni kutokana na ukodishaji wa Bohari na Majengo ya Serikali; na

iv. Kukamilisha mapitio ya Sheria ya Mitaji ya Umma nambari 4 ya mwaka 2022 na kuanzisha Sheria mpya ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma nambari 6 ya mwaka 2022 ambayo imepitishwa na Baraza la Wawakilishi mnamo mwezi wa Septemba mwaka 2021.

**SF010202 - Programu Ndogo ya Usimamizi wa Ununuzi na Uhakiki wa Mali za Serikali**

**27.** **Mheshimiwa Spika,** Lengo la programu ndogo hii ni kuwepo kwa uwazi na usawa wa tathmini ya mali zinazonunuliwa, kutunzwa na kuondoshwa kwa kuzingatia taratibu za manunuzi na usimamizi wa Mali. Hadi Machi 2022, TZS 63.04 milioni zimetumika sawa

na asilimia 29 ya makadirio ya TZS 216 milioni kwa kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kusimamia uondoshwaji wa mali chakavu zikiwemo gari, matangi, waya na vifaa vya Ofisi chakavu vya Wizara na Taasisi za Serikali. Jumla ya TZS 485 milioni zimepatikana kutokana na mauzo ya mali chakavu hizo;
ii. Kufuatilia na kuimarisha Daftari la Kumbu kumbu za Mali za Serikali kwa kukusanya taarifa za jumla ya mali 35,461 zinazojumuisha gari, vifaa vya ofisi, samani, majengo na mifumo ya tehama ya Wizara na Taasisi za Serikali kwa kuzingatia alama tambuzi na kuziingiza katika Daftari la Kielektroniki la Mali za Serikali;
iii. Kuhakiki na kuthamini mali zaidi ya 500 za Serikali ikiwemo mashamba, majengo, gari, vifaa vya kielektroniki, samani za Wizara na Taasisi za Serikali na kutoa miongozo ya uondoshaji, ukodishaji na utunzaji; na
iv. Kupatiwa mafunzo watendaji thelathini (30) wa Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango ya Mfumo wa kielektroniki wa Daftari la Usimamizi wa Mali za Serikali (Electronic Asset Register System). Kazi ya usambazaji wa Mfumo na kutoa mafunzo kwa watendaji wa Wizara na Taasisi nyengine za Serikali inaendelea ili watendaji hao waweze kuutumia mfumo na kuzisimamia mali za Serikali kwa ufanisi zaidi.

**PF0103 – Programu Kuu ya Uendeshaji wa Uratibu wa Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango**

**28.** **Mheshimiwa Spika,** Lengo la programu hii ni kuimarisha uendeshaji wa shughuli za Sekta ya Fedha. Hadi Machi 2022, TZS 11.36 bilioni zimetumika sawa na asilimia 54 ya makadirio ya TZS 21.13 bilioni kwa mwaka. Programu hii inatekelezwa kupitia programu ndogo tatu zifuatazo:

**SF010301 - Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji wa Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango – Unguja**

**29. Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la programu hii ni kusimamia masuala ya uendeshaji wa Ofisi na kuimarisha mazingira bora ya kazi. Hadi Machi 2022, TZS 3.23 bilioni zimetumika sawa na asilimia 60 ya TZS 5.41 bilioni zilizopangwa kutumika kwa kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kuratibu uendeshaji wa vikao 18 vya kamati ya uongozi na kamati tendaji vyenye lengo la kusimamia na kutoa maamuzi mbali mbali yanayohusu uendeshaji na usimamizi wa Ofisi pamoja na Taasisi zake;
ii. Kuratibu vikao 17 vya Bodi ya Zabuni kwa ajili ya kusimamia manunuzi mbali mbali ambayo yamefanywa na Ofisi katika kipindi cha miezi 9;
iii. Kutoa udhamini wa masomo ya muda mrefu kwa wafanyakazi (21) na wafanyakazi 313 mafunzo ya muda mfupi katika fani zinazohusiana na kada zao Unguja na Pemba;
iv. Kutoa huduma za kiutawala na uendeshaji zikiwemo matengenezo madogo madogo ya Ofisi, pamoja na ununuzi wa vitendea kazi; na
v. Kuhakikisha huduma za mawasiliano zinapatikana kila wakati.

**SF010302- Programu Ndogo ya Mipango Sera na Utafiti wa Sekta ya Fedha**

**30. Mheshimiwa Spika,** Lengo la Programu ndogo hii ni kuwa na Mipango na Sera ya Sekta ya Fedha iliyo imara nchini itakayosaidia kukuza uchumi. Hadi Machi 2022, TZS 6.25 bilioni zimetumika sawa na asilimia 51 ya TZS 12.33 bilioni zilizokadiriwa kwa kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kuandaliwa kwa Rasimu ya Sheria ya Usimamizi wa Taasisi zinazotoa huduma ndogo za kifedha ambayo imewasilishwa katika Kamati ya Katiba na Sheria ya Baraza la Mapinduzi;

ii. Vikao viwili (2) vya uchambuzi wa Takwimu za Fedha za Serikali vimefanyika ambapo Wataalamu kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) kwa kushirikiana na EAST-AFRITAC wametoa mafunzo kwa kikosi kazi cha Takwimu za Kifedha za Serikali (GFS) juu ya uandaaji wa ripoti za Kitakwimu kwa mujibu wa majukumu ya Serikali (COFOG) lengo la mafunzo haya ni kuwa naTakwimu bora za kifedha za Serikali zinazoendana na wakati wa sasa;
iii. Kuratibu vikao 36 vya Bodi ya Rufaa na Baraza la Rufaa za Kodi la Zanzibar. Kesi (21) zinafanyiwa kazi. Kesi ishirini (20) zipo katika hatua ya majadiliano ya kutafuta suluhisho la maamuzi na kesi moja inaendelea kusikilizwa;
iv. Kupatiwa mafunzo Wafanyakazi hamsini (50) Unguja na Pemba ya Mpango wa muda wa kati wa matumizi (MTEF) pamoja na maeneo ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ili kuleta ufanisi wakati wa uandaaji wa mipango inayozingatia Ilani ya CCM ya mwaka 2020 - 2025;
v. Kuandaliwa kwa Mpango Mkakati wa Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango ambapo hatua iliyofikiwa ni kuidhinishwa na kamati ya uongozi ya Wizara kwa ajili ya utekelezaji; na
vi. Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa miradi na programu za Ofisi. Ripoti za ufuatiliaji huu ndizo zinazoakisi utolewaji wa fedha za maendeleo kwa Taasisi zetu.

**SF010303 - Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara -Pemba**

31. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo hii ina lengo la kuhakikisha shughuli zilizopangwa kwa Sekta ya Fedha Pemba zinatekelezwa. Hadi Machi 2022, TZS 1.8 bilioni zimetumika sawa na asilimia 55 ya makadirio ya TZS 3.39 bilioni kwa ajili ya kutekeleza shughuli kwa upande wa Pemba zifuatazo:
i. Kusimamia ukusanyaji wa mapato yasiyokuwa ya kodi kwa upande wa Pemba ambapo jumla ya TZS 150.2 milioni

zimeweza kukusanywa hadi Machi, 2022 ni sawa na asilimia 91 ya makadirio ya TZS 165.08 milioni;

ii. Kuwapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi watano (5) katika fani zinazohusiana na kada zao;

iii. Ufuatiliaji wa mapato ya kodi na yasiyo ya kodi ulifanyika ukiwa na lengo la kuongeza makusanyo ya Serikali ambapo wafanyabiashara sabiini na tisa (79) walifuatiliwa juu ya utoaji wa stakabadhi za kieletroniki na wizara na taasisi tisa (9) za Serikali;

iv. Ufuatiliaji wa taarifa za kifedha kwa Asasi za kiraia arobaini na tatu (43) ulifanyika ambapo Serikali imeweza kujua mchango wa Asasi hizo katika mzunguko wa uchumi;

v. Kuhakiki taarifa za Wastaafu 3399 wanaopokelea pencheni yao Ofisi ya Rais-fedha na Mipango Pemba kwa lengo la kuwatambua pamoja na kuweka taarifa zao katika mfumo wa kidijitali ili kurahisisha utoaji wa huduma;

vi. Wizara11 zilifanyiwa ufuatiliaji wa utekelezaji wa shughuli za uhasibu na ukusanyaji wa mapato ili kuboresha utendaji wa uhasibu katika wizara husika;

vii. Watendaji watatu (3) walishiriki vikao vya kikanda vinavyohusiana na masuala ya kodi ambapo vimewajengea uwezo wa kusimamia majukumu yao; na

viii. Uhakiki na Uwekaji wa alama tambuzi kwa Taasisi za Serikali umefanyika ambapo vituo vya Afya 68 na mali zake 3000 na Vituo vya Wizara ya Elimu 22 na mali zake 2393 vimetambuliwa kwa lengo la kuingiza taarifa katika Daftari la Kielektroniki la Mali za Serikali.

## F. UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA FUNGU F02 (MFUKO MKUU WA SERIKALI)

32. **Mheshimiwa Spika,** Mfuko Mkuu wa Serikali unatekeleza programu ya Usimamizi wa Mfuko Mkuu wa Serikali. Hadi Machi 2022, programu hii imetumia TZS 136.95 bilioni sawa na asilimia 65 ya

makadirio ya kutumia TZS 208.99 bilioni kwa mwaka. Mchanganuo wa matumizi ya Mfuko Mkuu wa Serikali hadi Machi 2021/2022 ni kama ifuatavyo:

i. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2021/2022 Mfuko Mkuu umelipa mafao ya Kiinua Mgongo ya TZS 28.23 bilioni zimelipwa kwa wastaafu 1,753 kuanzia mwezi wa Januari, 2021 hadi Machi, 2022 na pencheni TZS 23.48 bilioni kwa wastaafu wastani wa 14,707 kwa mwezi;
ii. Kulipa Riba na Mikopo jumla ya TZS 28.30 bilioni;
iii. Malipo ya TZS 16.98 bilioni yalitumika kwa wananchi 9,264 wenye mikataba yenye thamani ya TZS 23.77 bilioni ambao walipeleka fedha katika Kampuni ya Masterlife Microfinance. Serikali ilitumia kifungu cha matumizi ya dharura ili kuwarudishia amana (mtaji) wananchi wake kutokana na hali ilivyoathiri mwenendo wa uchumi wa wananchi. Kwa sasa Serikali inaendelea kufuatilia mali na kukusanya mali za wamiliki wa Kampuni hiyo ili kuziba nakisi ya fedha iliyochangiwa; na
iv. Matumizi mengine ya Serikali kupitia Mfuko Mkuu TZS 39.96 bilioni.

## G. UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA FUNGU F03

33. **Mheshimiwa Spika,** Programu za Fungu F03 ziko chini ya Tume ya Mipango ya Zanzibar ambayo ina majukumu yafuatayo:

i. Kuandaa na Kusimamia utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa na Kuitafsiri kwenye mipango ya kisekta kwa kipindi cha muda wa kati kwa kuzingatia idadi ya watu na mahitaji yake;
ii. Kufanya uchambuzi wa masuala ya kiuchumi na kijamii na kuishauri Serikali ipasavyo;
iii. Kuratibu sera za kitaifa na kisekta za upunguzaji wa umaskini nchini;
iv. Kusimamia upatikanaji na utoaji wa Takwimu Rasmi kwa maendeleo ya nchi;
v. Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Mipango ya Kitaifa na

Kimataifa;

vi. Kufanya Tafiti kwa masuala mbali mbali ya Kitaifa na sera za kijamii na kuhakikisha maana na matokeo ya Tafiti hizo zimetekelezwa katika kukuza uwezo wa Taifa kiuchumi, kijamii na kiteknologia; na

vii. Kufanya mapitio na tathmini juu ya uwezo wa watu na vifaa kwa Zanzibar kwa azma ya kukuza maendeleo yao, ufanisi na matumizi yenye kuleta tija.

34. **Mheshimiwa Spika,** Tume ya Mipango inatekeleza programu kuu tatu (3) zenye programu ndogo nane (8). Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Tume ya Mipango Zanzibar iliidhinishiwa jumla ya TZS 23.15 bilioni kwa matumizi ya kazi za kawaida mishahara na kazi za maendeleo. Hadi Machi 2022, Tume ya Mipango Zanzibar imepata na kutumia TZS 8.63 bilioni sawa na asilimia 37 ya makadirio kwa mwaka, ambapo TZS 1.33 bilioni ni mishahara na TZS 3.17 bilioni ni matumizi kwa kazi za maendeleo.

**PF0301 - Programu Kuu ya Kuratibu Mipango ya Kitaifa na Maendeleo ya Watendakazi**

35. **Mheshimiwa Spika,** Lengo la Programu hii ni kuimarisha uratibu wa mipango ya maendeleo ya kitaifa na kufanya ufuatiliaji na tathmini wa mipango hiyo. Katika kipindi cha Julai 2021-Machi 2022, programu hii imetumia TZS 2.85 bilioni sawa na asilimia 59 ya makadirio ya TZS 4.85 bilioni. Programu hii ina programu ndogo tatu (3) zifuatazo:

**SF030101 – Program Ndogo ya Uratibu wa Mipango ya Kitaifa na Kupunguza Umasikini**

36. **Mheshimiwa Spika,** Lengo la Programu ndogo hii ni kuimarisha maendeleo kutokana na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar. Hadi Machi, 2022 programu hii ilitumia TZS 1.63 bilioni sawa na asilimia 53 ya makadirio ya TZS 3.05 bilioni kwa mwaka kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kukamilisha Rasimu ya mwisho ya Mpango wa Maendeleo wa Muda wa Kati (ZADEP) 2021-2026, hatua inayofuata ni kuchapishwa na kusambazwa kwa wahusika kwa ajili ya utekelezaji. Mpango huu utatumika kuoanisha Mipango Mikakati ya Sekta ili utekelezaji wa shughuli zao ziendane na Mpango huu wa Kitaifa;
ii. Kukamilisha Rasimu ya pili ya Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar kwa lugha nyepesi – Kiswahili na Kiingereza (ZADEP 2021-2026), hatua inayofuata ni kuidhinishwa na kuchapishwa. Kukamilika Kwa uandaaji wa mpango huu kwa lugha nyepesi kutasaidia kuongeza uelewa wa (ZADEP) kwa jamii.
iii. Maadhimisho ya Wiki ya Kupambana na Umasikini Duniani mwaka 2021 kwa Unguja na Pemba yamefanyika ambapo jumla ya Makongamano mawili (2) yaliandaliwa kwa kushirikisha makundi mbali mbali yakiwemo ya wazee, vijana na watu wenye mahitaji maalumu kwa lengo la kuwashajiisha juu ya njia mbali mbali za kupambana na umasikini. Aidha vipindi viwili (2) vya Televisheni na viwili (2) vya Redio kuhusiana na maadhimisho hayo vimetayarishwa na kurushwa hewani; na
iv. Warsha tatu (3) za kujenga uwelewa wa Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050 kwa makundi na Taasisi mbali mbali Unguja na Pemba zimefanyika ikiwemo Wizara tano (5) na Taasisi zake, Taasisi binafsi na Asasi za kiraia za Mkoa wa Kaskazini Unguja. Aidha vipindi 3 vya Redio na 3 vya Televisheni vimetolewa kwa lengo la kujenga uelewa wa Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050.

**SF030102 - Programu Ndogo ya Maendeleo ya Watendakazi na Masuala ya Idadi ya Watu**

37. **Mheshimiwa Spika,** Lengo la programu ndogo hii ni kuratibu masuala ya idadi ya watu, ustawi wa mama na mtoto na masuala ya watendakazi kitaifa. Hadi Machi 2022, programu hii imetumia TZS 602.23 milioni sawa na asilimia 86 ya makadirio ya TZS 702.31 milioni kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kuandaa Rasimu ya Sera ya Kitaifa ya Maendeleo ya Rasilimali watu na idadi ya watu ambayo inaendelea kupatiwa maoni ya wadau kabla ya kuwasilishwa katika vikao vya ngazi za juu. Sera hii itaimarisha ufanisi wa watu katika kutoa huduma ndani na nje ya nchi;
ii. Uwekaji wa Taarifa katika mfumo, taarifa hizo ni pamoja na taarifa za watu wenye ulemavu; Takwimu za vizazi na vifo ili kutoa ripoti mbali mbali ikiwa pamoja na kusaidia uchapishaji wa vyeti vya kuzaliwa wilayani;
iii. Kuimarishwa kwa Mfumo wa kidijitali wa kuhifadhi taarifa za idadi ya watu kwa baadhi ya vipengele kuingizwa na vyengine kupunguzwa ili kupatikana mfumo bora na wenye ufanisi;
iv. Kutolewa mafunzo ya ujazaji wa daftari la shehia na ufuatiliaji wa wajumbe wa shehia 156 Unguja na Pemba ili waweze kukusanya taarifa kwa usahihi na ufanisi;na
v. Kuandaliwa kwa vikao vinne (4) vya wadau wa masuala ya idadi ya watu na taarifa za utekelezaji wake zimewasilishwa.

**SF030103 - Programu Ndogo ya Ufuatiliaji na Tathmini wa Mipango wa Maendeleo**

38. **Mheshimiwa Spika,** Lengo la programu ndogo hii ni kuratibu ufuatiliaji na tathmini wa shughuli zilizoainishwa katika mikakati ya maendeleo. Hadi Machi 2022, programu hii imetumia TZS 614.47 milioni sawa na asilimia 56 ya makadirio ya TZS 1.09 bilioni kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kukamilisha ripoti ya utekelezaji ya Agenda ya Afrika ya 2063 ambayo imehusisha taarifa za Kimataifa, Tanzania Bara na Zanzibar na imewekwa katika tovuti ya Umoja wa Afrika;
ii. Kupatiwa mafunzo wafanyakazi kumi na saba (17) ya muongozo wa kidigitali wa Ufuatiliaji na Tathmini ambayo yamewawezesha kuweka taarifa za miradi katika mfumo huo;
iii. Kushiriki kwa wahusika 111 kutoka Taasisi za Serikali, Asasi za Kiraia na Tasisi binafsi katika kongamano la pamoja la kujadili

utekelezaji wa Mipango ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa na kupendekeza Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali kuandaa mpango kazi wa kutatua changamoto za upatikanaji wa taarifa za Takwimu;

iv. Kuandaliwa kwa Sera ya Ufuatiliaji na Tathmini na hatua inayofuata ni kuwasilishwa katika kamati ya Makatibu Wakuu kwa ajili ya kuthibitishwa;

v. Ushiriki wa Wadau 200 kutoka Taasisi za Serikali katika majadiliano ya Ripoti ya Hiari ya Utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu kwa upande wa Zanzibar (Voluntary National Review); na

vi. Kufuatilia miradi ishirini na moja (21) Unguja na Pemba inayotekelezwa kupitia fedha za Mkopo nafuu kutoka Shirika la Fedha Duniani (IMF) na ripoti imetayarishwa.

**PF0302 – Programu Kuu ya Usimamizi wa Uchumi Mkuu, Tafiti na Takwimu**

39. **Mheshimiwa Spika,** Lengo la programu hii ni kuandaa Sera za kiuchumi na kufanya tafiti za kiuchumi na kijamii kutokana na Vipaumbele vya Taifa. Hadi Machi 2022, programu hii imetumia TZS 4.88 bilioni ambayo ni sawa na asilimia 33 ya makadirio ya mwaka ya TZS 14.58 bilioni. Programu hii ina jumla ya programu ndogo tatu (3) ambapo Utekelezaji wa programu hizo ni kama ifuatavyo:

**SF030201 - Programu Ndogo ya Ukuzaji wa Uchumi.**

40. **Mheshimiwa Spika,** Lengo la programu ndogo hii ni kuendeleza hali ya uchumi tulivu unaolenga kuongeza mapato ya ndani, kupunguza nakisi ya bajeti na mfumko wa bei. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 programu hii ilikadiriwa kutumia TZS 744.24 milioni. Hadi Machi 2022, programu imetumia TZS 161.90 milioni sawa na asilimia 22 ya makadirio kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kutolewa Ripoti kumi na mbili (12) za hali ya Uchumi kwa kipindi cha mwezi, robo mwaka, miezi sita (6) na mwaka.

Taarifa za ripoti hizi zimekuwa zikitumika kama rejea katika programu zetu mbali mbali;

ii. Kuhudhuria Vikao Saba (7) vya kamati ya wataalamu ya madeni Dodoma. Katika vikao hivyo, Miradi mbali mbali ilichambuliwa na kutolewa mapendekezo kwa kamati ya Kitaifa yenye kutoa ushauri kwa Waziri anaehusika na masuala ya fedha kwa ajili ya kutoa maamuzi;

iii. Wafanyakazi watano (5) wamepatiwa mafunzo ya wiki moja (1) kwenye matumizi ya Programu ya "E view" yaliyofanyika Benki Kuu ya Tanzania Dar es salaam. Mafunzo hayo yameimarisha utoaji wa utabiri wa mfumko wa bei wa Zanzibar kwa kila mwezi;

iv. Kushiriki mikutano miwili (2) ya Jumuiya ya Afrika Mashariki inayohusiana na kuboresha mikakati na mipango ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Mikutano hiyo imesaidia kuelewa mwelekeo wa Mipango ya Afrika ya Mashariki kwa siku zijazo ambazo nchi wanachama zinapaswa kuzingatia.

**SF030202 - Programu Ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Shughuli za Takwimu Zanzibar**

41. **Mheshimiwa Spika,** Lengo la programu hii ni kuimarisha Takwimu na Viashiria vya Kiuchumi na Kijamii kwa Mipango ya Maendeleo. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Programu hii ilikadiriwa kutumia TZS 12.78 bilioni. Hadi Machi 2022, ilitumia TZS 4.59 bilioni sawa na asilimia 36 ya makadirio kwa kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kutolewa ripoti hamsini na mbili (52) za kiuchumi na kijamii ikiwemo ripoti za kila mwezi za Faharisi ya Bei ya Mlaji (Consumer Price Index- CPI), Ripoti za Watalii wanaongia nchini (Tourism Arrival), Ripoti za Takwimu za matukio ya Ajali na Makosa ya Barabarani, Ripoti ya Takwimu za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia kwa wanawake na watoto pamoja na Ripoti za robo mwaka za Pato la Taifa (Quartely GDP reports);

ii. Kukamilika kwa miongozo miwili (2) ya mgawanyo wa shughuli za kiuchumi na kijamii (ISIC) na muongozo wa tafsiri

za misamiati ya kitakwimu kwa ajili ya kusimamia viwango na mifumo ya kitakwimu;

iii. Kukamilika kwa kazi ya uchambuzi wa Viashiria vya Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) vinavyoweza kutumika kwa Zanzibar kwa kuvitayarishia 'meta data';

iv. Kuratibu na kusimamia vikao vitano (5) vya Bodi ya Takwimu, Kikao kimoja (1) cha Kamati ya Ukaguzi na vikao vinne (4) vya Bodi ya Zabuni; na

v. Kuwapatia mafunzo Watumishi 47 katika fani ya Takwimu, Watumishi saba (7) mafunzo ya muda mrefu na watumishi arubaini (40) mafunzo ya muda mfupi.

**SF030203- Programu Ndogo ya Uratibu wa Tafiti na Ubunifu**

**42.** **Mheshimiwa Spika,** Lengo la programu ndogo hii ni kuratibu na kusimamia masuala ya tafiti nchini. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 programu hii ilikadiriwa kutumia TZS 1.06 bilioni. Hadi Machi 2022, programu hii imepatiwa TZS 125.50 milioni, sawa na asilimia 12 ya makadirio kwa mwaka kwa kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kuratibu Tafiti nne (4) tafiti hizo ni:

a) Tija ya Kiuchumi ya Idara Maalum na Mchango wao katika Ukuaji Endelevu wa Uchumi wa Jamii. Utafiti huu unalenga kuonyesha maeneo muhimu ya Uwekezaji na kukuza Uchumi katika Vikosi vya SMZ vya Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) na Chuo cha Mafunzo hatimae kuongeza tija katika uzalishaji wa kilimo na mifugo;

b) Athari za Kifafa cha Mimba/ Uzazi kwa baadhi ya wanawake wenye ujauzito. Utafiti huu umelenga kuleta ushahidi wa kuimarisha afya za kinamama waja wazito waliopata kifafa cha mimba wakati wa ujauzito na hivyo kupunguza vifo vya kinamama;

c) Kutathmini uwezo wa Watumishi wa Sekta za Umma Zanzibar. Utafiti huu umelenga kuibua mapendekezo ya aina ya mafunzo na ujuzi ya muda mrefu na mfupi ambayo watahitaji Watumishi wa Sekta za Umma kuimarisha

utendaji wa majukumu yao; na

d) Teknolojia mpya ya kilimo mjumuisho cha ufugaji samaki, kuku, ukulima wa mboga mboga na ufugaji nyuki kwa pamoja kwa ajili ya kuimarisha Maisha ya jamii ya Zanzibar. Utafiti huu unalenga kuunganisha Sekta ya Uchumi wa Buluu na Kilimo kwa kutoa ushahidi wa kilimo mjumuisho cha samaki, kuku na mbogamboga na hivyo kutumia eneo dogo na kuimarisha uchumi wa jamii.

ii. Kupatiwa mafunzo watumishi 68 kutoka taasisi mbalimbali za Serikali kuhusu uandishi wa maandiko ya kutafuta fedha, kuchambua matokeo ya tafiti na kufanya tathmini za miradi kwa lengo la kuimarisha utendaji wao;

iii. Kuandaliwa Andiko moja (1) la Mradi wa Miundombinu ya Kuimarisha Uchumi wa Buluu na Uhifadhi wa Taarifa za Tafiti kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA), Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi, Idara ya Uvuvi. Mradi huu upo katika hatua ya uzinduzi ili uweze kuanza utekelezaji wake;

iv. Kupatiwa mafunzo ya ziara Dodoma watendaji wakuu saba (7) juu ya usimamizi wa Bioanuai 'Biosafety'. Hii imesaidia kuboresha rasimu ya muongozo wa usimamizi wa usalama wa matumizi ya 'Bioanuai' (Zanzibar Biosafety Framework) kwa binaadamu, wanyama na mazingira kutokana na athari zinazoweza kusababishwa na matumizi ya bioteknolojia 'biosafety'. Mafunzo hayo yamewezesha kuandaa rasimu ya muongozo wa Tafiti za Ndani;

v. Vikao kazi vitatu (3) vimefanyika vya kuandaa muongozo wa usimamizi wa fedha/ruzuku za tafiti na ubunifu kwa kushirikiana na Mtaalamu kutoka Tume ya Taifa ya sayansi na teknolojia ambapo rasimu ya awali imekamilika na itapelekwa kwa wadau na ngazi mbali mbali kwa maoni;

vi. Kuandaliwa na kuwasilishwa kwa wadau Mihutasari mitatu (3) ya Sera inayohusiana na Uchumi wa Buluu. Mihutasari yenyewe ni:

a) Muhtasari wa Kuimarisha Uvuvi Endelevu kwa Wadau,

b) Muhtasari wa athari zinazosababishwa na binaadamu juu ya rasilimali za baharini na
c) Muhtasari wa njia bora za kuongeza uzalishaji wa mwani, kuboresha biashara ya mwani na kuongeza thamani na usindikaji wa mwani; na

vii. Kukusanya Taarifa za tafiti mia moja na hamsini (150) na kuhifadhiwa katika kanzi data ya idara ili kuchambuliwa na matokeo kuwasilishwa Serikalini na kwa wadau kwa ajili ya kusaidia kutoa maamuzi na kutatua changamoto za kiuchumi na kijamii.

**PF0303 - Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Tume ya Mipango**

43. **Mheshimiwa Spika,** Lengo la programu hii ni kusimamia shughuli za utendaji na utumishi ndani ya Tume ya Mipango na kuhakikisha kazi zinatekelezwa kwa ufanisi. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 programu hii ilikadiriwa kutumia TZS 3.72 bilioni. Hadi Machi 2022, program hii imetumia TZS 905.69 milioni ambayo ni sawa na asilimia 24 ya makadirio kwa mwaka. Programu hii ina jumla ya programu ndogo mbili (2) ambapo Utekelezaji wa programu hizo ni kama ifuatavyo:

**SF030301 - Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Mipango**

44. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Programu hii ilikadiriwa kutumia TZS 3.18 bilioni. Hadi Machi 2022, programu hii ilitumia TZS 634.63 milioni sawa na asilimia 20 ya makadirio kwa mwaka kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kutoa huduma za kiutawala na uendeshaji zikiwemo matengenezo ya Ofisi, gari, ununuzi wa mafuta, vifaa vya kuandikia, pamoja na ununuzi wa vitendea kazi;
ii. Kuratibu Vikao kumi na tatu (13) vikiwemo: Kikao kimoja (1)

cha Tume ya Mipango, vinne (4) Kamati ya Wataalamu, vinne (4) vya Bodi ya Zabuni na Tathmini na Vitatu (3) vya Ukaguzi wa hesabu za ndani; na

iii. Kupatiwa mafunzo Wafanyakazi thelathini na tatu (33) Unguja na Pemba kati ya hao wafanyakazi kumi (10) mafunzo ya muda mrefu na wafanyakazi ishirini na tatu (23) mafunzo ya muda mfupi katika fani zinazohusiana na kada zao.

**SF030302- Programu ya Uratibu na Utekelezaji wa shughuli za Tume ya Mipango Pemba**

45. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Program hii ilikadiriwa kutumia TZS 538.29 milioni. Hadi Machi 2022, programu ilipatiwa na kutumia TZS 271.06 milioni sawa na asilimia 50 ya makadirio kwa kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kuratibu shughuli za utawala na uendeshaji ikiwemo kusimamia huduma za uendeshaji, likizo pamoja na mafunzo ya ndani; na

ii. Kuratibu shughuli za Idara zilizo chini ya Tume ya Mipango kwa kushirikiana na Ofisi kuu Unguja na ripoti tano (5) zimetayarishwa.

## H. UTEKELEZAJI WA MIRADI YA OFISI YA RAIS - FEDHA NA MIPANGO

46. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango imesimamia na kutekeleza Miradi ifuatayo:

i. **Mradi wa Mageuzi ya Usimamizi wa Fedha za Umma** (PFMRP-V) Lengo la mradi huu ni kuleta Mageuzi katika Usimamizi wa Fedha za Umma chini ya Ufadhili wa Norway, Denmark na DFID kupitia Mfuko wa Pamoja wa Ufadhili. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Mradi huu ulikadiriwa kutumia TZS 1.64 bilioni. Hadi Machi 2022, Mradi umetumia TZS 468.96 milioni sawa na asilimia 30 ya makadirio ya mwaka kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:

a) Kuanzisha Mfumo wa taarifa za Bajeti na Matumizi (BAMAS) ambapo pamoja na mambo mengine, imewapatia mafunzo watumishi mbali mbali juu ya matumizi yake;
b) Kuanzisha Mfumo wa manunuzi wa kielektroniki (E-Procurement). Hatua iliyofikiwa kwa sasa ni Mshauri Elekezi anaendelea kukusanya taarifa zinazohitajika katika mfumo huo kwa kushirikiana na Mamlaka ya Usimamizi wa Manunuzi ya Umma na Wakala wa Serikali Mtandao;
c) Kufanya manunuzi ya server za mifumo kwa Ofisi ya Serikali Mtandao (E-Government Agency), kwa Ofisi ya ZURA na Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango;
d) Kutolewa mafunzo ya Mfumo wa manunuzi wa kielektroniki (E- Procurement) kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati za Baraza la Wawakilishi kwa lengo kukuza ufanisi kusimamia Serikali katika utekelezaji wa majukumu yao;
e) Kutoa Mafunzo ya kitaalamu ya utumiaji wa mfumo wa (ZAN-MALIPO) kwa taasisi 152 za Unguja na Pemba; na
f) Mpango Mkakati wa Usimamizi wa Fedha za Umma (PFM Strategic Plan) umekamilika na utekelezaji wake utaanza mwaka wa fedha 2022/2023.

ii. **Mradi wa Uimarishaji Rasilimali za ndani na Usimamizi wa Mali asili** (ISP - DRMNRG) Lengo la Mradi huu ni kuimarisha upatikanaji wa rasilimali za ndani na usimamizi wa maliasili chini ya ufadhili wa Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB). Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Mradi huu ulikadiriwa kutumia TZS 3.88 bilioni. Hadi Machi 2022, mradi umetumia TZS 539.22 milioni sawa na asilimia 14 ya makadirio ya mwaka kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:
a) Kujenga hamasa juu ya makusanyo ya ndani;
b) Kutoa Mafunzo kwa wataalamu elekezi wa kodi;
c) Kufanya malipo kwa ajili ya Contact Centre ya ZRB;

d) Kusaidia mfumo wa uendeshaji wa kazi za ZURA; na
e) Kutoa mafunzo ya usimamizi wa mapato kwa TRA.

iii. **Mradi wa Uimarishaji Utawala bora** (ISPGG III) Lengo la mradi huu ni kukuza uchumi kwa kuimarisha utawala bora wa kiuchumi na kifedha kupitia ufanisi wa usimamizi wa fedha za umma na mazingira bora ya biashara chini ya ufadhili wa Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB). Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, mradi huu ulikadiriwa kutumia TZS 1.506 bilioni. Hadi Machi 2022, mradi umetumia TZS 1.502 bilioni kutekeleza shughuli zifuatazo:
a) Kutengeneza mfumo wa *"National Online Registration System"* kwa taasisi za BLRC, BPRA, ZCT, na ZIPA. Mfumo huo tayari umeanza kazi katika Taasisi hizo kwa hatua ya awali; na
b) Kuandaa Miongozo ya Uwekezaji *"Investment Regulations"* kwa ZIPA.

iv. **Mradi wa Ujenzi wa Ofisi za Serikali** Lengo la Mradi huu ni kuimarisha ufanisi wa utendaji Serikalini kwa kutengeneza Ofisi mbali mbali. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Mradi ulikadiriwa kutumia TZS 76.4 bilioni. Hadi Machi 2022, mradi umetumia TZS 2.4 bilioni sawa na asilimia 3 ya makadirio ya mwaka kwa ajili ya Ujenzi wa Mahkama Kuu iliyopo Tunguu pamoja na Ununuzi wa Vifaa vya samani vya Ofisi ya Mahakama na Ujenzi wa jengo la SMIDA la Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda liliopo Maruhubi.

v. **Mradi wa Ukuzaji Uchumi Jumuishi** (Boosting Inclusive Growth for Zanzibar (BIG -Z)) Lengo la Mradi huu ni kuimarisha hali ya maisha na kukuza maendeleo ya Kiuchumi katika maeneo ya Unguja na Pemba kwa kuimarisha miundombinu na huduma, uhifadhi wa urithi na usimamizi jumuishi wa miji chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia. Programu imeanza utekelezaji wake mwezi wa Disemba 2021 ambapo kwa mwaka wa fedha

2021/22 ilikadiriwa kutumia TZS 5.7 bilioni. Hadi kufikia mwezi Machi 2022, Programu iliingiziwa jumla ya TZS 8.8 bilioni sawa na asilimia 154 ya makadirio ya nusu mwaka. Hadi tarehe 30 Machi 2022, jumla ya TZS 17.7 milioni zimetumika kwa ajili ya uendeshaji wa mradi sawa na asilimia 0.2 ya fedha zilizopatikana katika kipindi cha mwezi Machi 2022. Kazi zilizofanyika ni pamoja na:

a) Kuratibu vikao kazi 12 na kikosi kazi cha wataalamu wa taasisi zinazotekeleza Mradi (Technical working groups) kwa ajili ya kukamilisha Hadidu rejea na nyaraka za zabuni.
b) Kushiriki kongamano la kutathmini utekelezaji wa miradi inayofadhiliwa na Benki ya Dunia Tanzania kwa lengo la kuongeza uzoefu katika kusimamia miradi inayofadhiliwa na Benki ya Dunia, hivyo maofisa wanaosimamia mradi huu (BIG-Z) wamepata kujifunza na kuongeza uzoefu katika masuala yanayohusiana na ununuzi, usimamizi wa fedha, mikataba pamoja na uratibu wa miradi.
c) Kutoa mafunzo ya Sheria na Kanuni za Ununuzi za Benki ya Dunia kwa wajumbe wa Bodi ya Zabuni ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango. Mafunzo haya yamewaongezea uwezo wajumbe wa Bodi ya Zabuni na pamoja na mbinu za kuimarisha usimamizi wa miradi ili kuleta ufanisi zaidi; na
d) Ununuzi wa vitendea kazi vya Ofisi (stationaries) pamoja na mafuta kwa ajili ya gari inayotumiwa na Mradi.

vi. **Mradi wa Mpango wa Kuimarisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania** (MKURABITA) Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 programu hii ilikadiriwa kutumia TZS 2 bilioni. Hadi Machi 2022, programu imetumia TZS 1.01 bilioni ambazo ni sawa na asilimia 51 ya makadirio ya mwaka. Programu hii imelenga kuwakwamua wananchi na umasikini kupitia urasimishaji wa biashara na ardhi ili ziweze kutumika katika

kujiletea maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Kazi zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa kituo jumuishi cha urasimishaji biashara Mkokotoni, kuwapatia mafunzo wajasiriamali mia mbili hamsini (250) juu ya masuala ya kuhifadhi taarifa za kifedha pamoja na ufunguaji wa accounts ili kusaidia kuinuka kiuchumi kwa kupata uwezo wa kusajili biashara zao na kupata mikopo katika taasisi za kifedha.

vii. **Mradi wa Uendelezaji Takwimu** (ZSDP) Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 mradi huu ulikadiriwa kutumia TZS 9.15 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo (AfDB, UNFPA, EU, USAID, UN-Wowen na Basket Fund). Hadi Machi 2022, mradi umetumia jumla ya TZS 3.2 bilioni ambazo ni sawa na asilimia 35 ya makadirio ya mwaka kwa ajili ya kutekeleza shughuli zikwemo:

a) Kukamilisha na kutoa ripoti ya utafiti wa watu wenye uwezo wa kufanya kazi ya mwaka 2020/2021. Matokeo yanaonesha kwamba kiwango cha ukosefu wa ajira kwa mwaka 2020/2021 kimeongezeka hadi kufikia asilimia 19.6 ukilinganisha na mwaka 2014 (asilimia 14) ambapo kwa wanaume ni asilimia 10.3 na wanawake asilimia 29;

b) Kukamilisha na kutoa ripoti ya Sensa ya Kilimo na Mifugo ya Mwaka 2019/2020 ripoti hiyo imeonesha kuongezeka kwa kaya zinazojishughulisha na kilimo kutoka kaya 132,193 mwaka 2007/2008 hadi kaya 180,220 mwaka 2019/2020 ikiwa ni ongezeko la asilimia 36;

c) Kukamilisha zoezi la uorodheshaji wa maeneo ya kuhesabia watu kwa ajili ya utafiti wa hali ya afya wa mama na mtoto ambapo maeneo 90 yameorodheshwa Unguja na Pemba; na

d) Kukamilisha zoezi la Sensa ya Majaribio ya Watu na Makaazi ya Mwaka 2022 pamoja na kazi za utengaji wa maeneo ya kuhesabia watu (Emuneration Areas) kwa Zanzibar.

Orodha ya miradi inayosimamiwa na Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango inaonekana katika **Kiambatisho Namba 3.**

## I. UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA TAASISI ZA OFISI YA RAIS - FEDHA NA MIPANGO JULAI 2021 - MACHI 2022.

### a) Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB)

47. **Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB), ni Wakala Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wa kukusanya mapato yatokanayo na Kodi. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, ZRB ilikadiriwa kukusanya TZS 525.10 bilioni. Hadi Machi 2022, Bodi ya Mapato imekusanya TZS 275.17 bilioni sawa na asilimia 52 ya makadirio ya mwaka.

48. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa matumizi, Bodi ya Mapato Zanzibar ilikadiriwa kutumia TZS 17.084 bilioni kwa ajili ya kutekeleza kazi zake za kawaida na kazi za maendeleo. Hadi Machi 2022, Bodi ya Mapato Zanzibar imetumia TZS 7.528 bilioni sawa na asilimia 44 ya makadirio ya mwaka. Kati ya Fedha hizo TZS 0.2 bilioni zimetumika kwa kazi za maendeleo na TZS 7.32 bilioni zimetumia kwa kazi za kawaida. Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na:-

  i. Kufuatilia ugomboaji wa madeni ya TZS 20 bilioni yaliyokuwa hayajalipwa kutoka kwa walipa kodi mbalimbali. Kwa kipindi cha miezi tisa jumla ya TZS 17.34 bilioni sawa na asilimia 89 ya madeni yote yalilipwa;
  ii. Kusajili walipakodi 4,231 katika mfumo wa kutolea risiti za kielektroniki (VFMS), mashine 4,670 za kutolea risiti (POS) ziliuzwa kwa wafanyabiashara. Aidha, Jumla ya mauzo TZS 648.89 bilioni yalifanyika na kodi iliokusanywa ni TZS 66.08 bilioni;
  iii. Kuunganisha mfumo wa VFMS na mifumo mengine, mfumo huo umeunganishwa na selcom company kwa ajili ya meseji za simu, Idara ya Uhamiaji kwa ajili ya taarifa za wageni, na

mfumo wa ZITAS kwa ajili ya kupata taarifa za walipakodi;

iv. Kuongeza ubunifu katika Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwa mfumo kwa kutoa ripoti kwa mgeni wakati wa kutoka hotelini ambayo itahakikiwa uwanja wa ndege (Checkout report), zawadi kwa wanaodai risiti kwa wingi (reward system), aidha mfumo kuweza kutumika katika vifaa mbalimbali vya kielektroniki (virtual system);

v. Kutoa mafunzo na elimu ya matumizi ya mfumo wa VFMS kwa walipakodi wasiopungua 4,231, Aidha, video zinazoelekeza matumizi ya mfumo huo zimetengezwa;

vi. Katika kipindi cha miezi tisa, walipakodi wapya 1,622 walisajiliwa katika wigo tofauti sawa na asilimia 54 ya makadirio ya walipakodi 3,000 waliotarajiwa kusajiliwa kwa mwaka 2021/2022;

vii. Kaguzi tatu (3) zilifanyika katika kampuni za simu na kulipwa kodi ya TZS 1.7 bilioni; na

viii. Kufanya kaguzi kwa hoteli kubwa kumi na mbili (12) ambapo jumla ya TZS 5.80 bilioni zimegombolewa.

**b) Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)**

**49. Mheshimiwa Spika,** Katika Kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi 2022 Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) imekusanya TZS 256.36 bilioni ya makadirio ya kukusanya TZS 413.1 bilioni ikiwa ni sawa na asilimia 62 ya lengo la kipindi hicho.

**c) Mfuko wa Barabara (ZRF)**

**50. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Mfuko wa Barabara Zanzibar umeendelea na jukumu lake la kudumisha utaratibu madhubuti wa utunzaji wa fedha zinazokusanywa kwa ajili ya matengenezo ya barabara pamoja na kuimarisha utaratibu wa kukagua matumizi ya fedha hizo kwa dhamira ya kuwa na miundombinu endelevu.

51. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Mfuko wa Barabara uliidhinishiwa TZS 14.64 bilioni. Kati ya fedha hizo TZS 14.29 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na TZS 344.3 milioni kwa ajili ya malipo ya mishahara. TZS 12.86 bilioni zilitengwa kwa kazi za matengenezo ya barabara sawa na asilimia 90 ya TZS 14.29 zilizoidhinishwa kwa matumizi mengineyo. Kazi hizo zinatekelezwa na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kupitia Wakala wa Barabara Zanzibar. Aidha, TZS 1.77 bilioni zilitengwa kwa kazi za uendeshaji wa Mfuko.

52. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa matumizi ya Mfuko wa Barabar hadi Machi 2022, TZS 615 bilioni zimetumika sawa na asilimia 55 ya TZS 11.17 bilioni. Kati ya matumizi hayo, TZS 5.46 bilioni zililipwa kwa kazi za matengenezo ya barabara na TZS 590 milioni zililipwa kwa kazi za uendeshaji wa Mfuko.

53. **Mheshimiwa Spika,** Barabara zilizohusika na matengenezo hayo ni Kipapo –Mgelema – Wambaa (9.3km) Micheweni – Maeneo huru ya uwekezaji (2.4 km) Njia za waendao kwa miguu, Uwanja wa Ndege-Mazizini Barabara ya ZRB (3.1km), Kinduni- Kichungwani – Kitope (4.0 km) na Sharifumsa – Mwanyanya – Bububu Skuli (3.8 km). Aidha matengenezo mbalimbali ya kawaida yamefanyika yakiwemo, uzibaji wa mashimo, ununuzi wa zana nzito na usimamizi wa kazi.

### d) Mamlaka ya Manunuzi na Uondoaji wa Mali za Umma (ZPPDA)

54. **Mheshimiwa Spika,** Lengo la Mamlaka ya Manunuzi na Uondoaji wa Mali za Umma ni kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma, nambari 11 ya mwaka 2016. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Mamlaka imepangiwa kukusanya TZS 444.42 milioni kutoka katika vyanzo vyake mbali mbali vya mapato. Hadi Machi 2022, Mamlaka imekusanya TZS 144 milioni ambayo ni sawa na asilimia 33 ya makadirio ya mwaka.

**55. Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa matumizi, hadi Machi 2022, Mamlaka imetumia TZS 761.66 milioni sawa na asilimia 35 ya kupokea ruzuku ya TZS 2.15 bilioni kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kukagua taasisi nunuzi za umma. Ukaguzi wa Taasisi 30 za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimekaguliwa kwa ajili ya kuhakikisha zinakidhi matakwa ya kisheria (Compliance) na thamani halisi ya fedha katika ununuzi (Value for money in Procurement) ili kuhakikisha taratibu za kisheria zinafuatwa pamoja na upatikanaji wa ubora wa bidhaa unaoendana na thamani halisi ya fedha;

ii. Kuchunguza Miamala ya Ununuzi juu ya ukiukwaji wa taratibu za manunuzi kwa Taasisi mbili za umma ambazo ni Taasisi ya Viwango, Zanzibar (ZBS) na Chuo cha Taifa Cha Zanzibar (SUZA) ambapo uchunguzi huo umebaini ukiukwaji mkubwa wa sheria ya ununuzi;

iii. Kupewa mafunzo taasisi 12 za umma juu ya Sheria na Kanuni ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma na miongozo ili kuimarisha utendaji katika taasisi hizo;

iv. Mamlaka imepokea mipango 90 ya manunuzi ya mwaka kwa Taasisi nunuzi kati ya 93 ya taasisi za umma, taasisi 3 hazikuwasilisha mipango yao ya ununuzi;

v. Kupokea malalamiko ya watoa huduma jumla ya malalamiko mawili (2) yalipokelewa kutoka kwa Wazabuni kwa kutokuridhika na hatua za zabuni kutoka Chuo cha Mafunzo na Shirika la Meli Zanzibar. Malalamiko hayo yalifanyiwa kazi na kupatiwa ufumbuzi kwa pande zote zinazohusika;

vi. Wafanyakazi wanne (4) wa Mamlaka wamefaidika kupata utaalamu na uzoefu wa kiutendaji kupitia mashirikiano baina ya Mamlaka ZPPRA na PSPTB za Tanzania Bara;

vii. Kukagua taarifa za manunuzi za miradi mbali mbali iliyopatiwa fedha za kupambana na maradhi ya Uviko -19 ambapo miradi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Wizara ya Maji Nishati na Madini pamoja na Wizara ya Afya imekaguliwa hadi

Aprili, 2022; na

viii. Kupitia Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma nambari 11 ya 2016 ambapo Mamlaka imeanza na kazi ya kukusanya maoni ya rasimu ya sheria mpya ya ununuzi.

**e) Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF)**

**56. Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) umeendelea kutoa huduma kwa Wanachama wake kwa kukusanya michango yao na kuwekeza fedha hizo katika miradi salama na yenye faida kwa lengo la kulipa mafao kwa Wanachama muda unapofika kwa mujibu wa Sheria ya Mfuko Nambari 10 ya mwaka 2016.

**57. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Mfuko ulikadiriwa kukusanya TZS 82.80 bilioni kutoka katika vyanzo vikuu viwili. Hadi Machi 2022, Mfuko ulikusanya TZS 87.51 bilioni sawa na asilimia 105.69 ya makadirio ya mwaka. Kati ya mapato hayo michango ya wanachama ni TZS 70.08 bilioni sawa na asilimia 100 ya makadirio ya TZS 69.72 bilioni na mapato kutoka katika uwekezaji wa mfuko ni TZS 17.43 bilioni sawa na asilimia 134 ya TZS 13.04 bilioni makadirio ya mwaka.

**58. Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa matumizi Mfuko ulikadiriwa kutumia TZS 32.29 bilioni, kati ya fedha hizo TZS 19.18 bilioni ni malipo ya kiinua mgongo, TZS 190 milioni ni malipo ya mafao ya Uzazi ya Wanachama wa Mfuko, TZS 10.97 bilioni kwa ajili ya kulipa Pencheni ya Wanachama na TZS 1.94 ni malipo kwa ajili ya kulipa marejesho kwa Wanachama. Hadi Machi 2022, Mfuko umetumia TZS 35.23 bilioni sawa na asilimia 109.10 ya makadirio ya TZS 32.29 ya mwaka. Kati ya fedha hizo malipo ya kiinua mgongo ni TZS 18.63 bilioni, malipo ya Mafao ya Uzazi kwa wanachama ni TZS 170 milioni, malipo ya Pencheni kwa Wanachama wa Mfuko ni TZS 14.02 bilioni na malipo kwa ajili ya marejesho ya Wanachama wa mfuko ni TZS 2.41 bilioni.

### f) Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ)

59. **Mheshimiwa Spika,** Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) ni Taasisi inayomilikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa asilimia 100. PBZ inafanya kazi za kibenki kama Benki nyengine za kibiashara zinazofanya kazi Zanzibar. Benki hii inatoa huduma za benki ya kawaida (Conventional) na huduma za Benki ya Kiislam (Islamic Banking).

60. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022, PBZ ilikadiriwa kukusanya kutoka vyanzo vyake vya riba na visivyo na riba TZS 76.87 bilioni na kufanikiwa kukusanya TZS 80.18 bilioni sawa na asilimia 104 ya makusanyo ya kipindi hicho.

61. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa matumizi Benki ilitumia TZS 61.92 bilioni sawa na asilimia 119 ya makadirio ya TZS 52.16 bilioni iliyojipangia kwa kipindi cha tathmini.

62. **Mheshimiwa Spika,** Hadi Machi 2022, mikopo iliyotolewa katika sekta tofauti inaonesha kukuwa kwa asilimia 24% kutoka TZS 520,264 milioni Julai 2021 hadi TZS 646,404 milioni Machi 2022. Rasilimali (Assets) zimeendelea kukua na kufikia TZS 1.062 bilioni ukilinganisha na TZS 832 bilioni kwa mwezi wa Julai, 2021 ambapo ni ongezeko la asilimia 28. Aidha Amana za PBZ zimeongezeka kwa asilimia 44% na kufikia TZS 881 bilioni hadi Machi 2022 kulinganisha na TZS 610.27 bilioni zilizorekodiwa Machi 2021 na Mtaji wa benki hadi Machi 2022 ni TZS 127 bilioni, ni ongezeko la asilimia 5 kutoka Julai 2021 (TZS. 121 bilioni).

### g) Shirika la Bima (ZIC)

63. **Mheshimiwa Spika,** Shirika la Bima linaendelea na kazi ya kutoa huduma za bima kwa wateja pamoja na kuongeza Mapato kutoka vyanzo vyake mbali mbali. Katika kipindi cha miezi tisa Julai, 2021-

Machi 2022, Shirika limekusanya TZS 21.20 bilioni sawa na asilimia 68 ya makadirio ya kukusanya TZS 31 bilioni kwa mwaka.

**64.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa matumizi katika kipindi cha Julai hadi Machi, 2022 Shirika limeweza kutumia TZS 5.70 bilioni ikiwa ni matumizi ya kawaida sawa na asilimia 37 ya makadirio ya matumizi ya kawaida yaliyokadiriwa kwa kipindi cha mwaka ambayo ni TZS 15.5 bilioni.

**65.** **Mheshimiwa Spika,** Shirika la Bima, katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022 limeweza kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kulipa madai halali yaliyowasilishwa na yaliyohakikiwa ya TZS 3.5 bilioni kutoka kwa wateja wake walioathirika na majanga mbalimbali ya ajali;
ii. Kulipa ujira wa TZS 2.1 bilioni kwa Mawakala na Madalali 177 wanaofanya biashara ya kuuza bima kwa niaba ya Shirika; na
iii. Kutoa gawio kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar lenye jumla ya TZS 600 milioni sawa na asilimia 75 ya makadirio ya TZS 800 milioni kutokana na faida iliyopatikana mwaka wa fedha 2020.

## J. MWELEKEO WA BAJETI YA OFISI YA RAIS- FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA WA FEDHA 2022-2023

### Vipaumbele vya Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango

**66.** **Mheshimiwa Spika,** Baada ya kuzingatia miongozo ya Nchi ikiwemo Dira ya Maendeleo 2050, Mpango Mkakati wa Maendeleo wa muda wa kati ZADEP 2021 – 2026, Ilani ya Uchaguzi wa CCM ya mwaka 2020- 2025 na Hotuba ya Mheshimiwa Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi aliyoitoa katika uzinduzi wa Baraza la Kumi la Wawakilishi. Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango imekusudia kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:

i. Kusimamia ukusanyaji wa mapato ya Serikali ya **TZS 2.491 trilioni;**

ii. Kuimarisha udhibiti wa matumizi ya fedha kupitia Mifumo ya Kielektroniki;
iii. Kufanya Sensa ya Watu na Makazi ya 2022;
iv. Kukamilisha Mkakati wa Kifedha kwa Mpango wa Maendeleo (ZADEP) na Mpango wa Utekelezaji wake;
v. Kusimamia matumizi ya mfumo wa kurikodi taarifa za watu sambamba na daftari la Shehia;
vi. Kuandaa Sera ya Taifa ya Rasilimali Watu Zanzibar;
vii. Kutayarisha Mpango wa Utekelezaji wa Ajenda ya Utafiti ya Zanzibar 2021-2026;
viii. Kuratibu utayarishaji wa upembuzi yakinifu (Feasibility Study) kwa Sekta kuu za Uchumi na Jamii katika maeneo yakiwemo Uchumi wa Buluu, Viwanda na Miundombinu ya Usafirishaji;
ix. Kufanya uchambuzi wa Matokeo ya Tafiti kumi (10) katika maeneo ya Uchumi wa Buluu, Utalii, Uchumi na Fedha, Utoaji wa huduma, kilimo na Ajira na kuwasilisha Serikalini na kwa wadau kwa lengo la kufanya maamuzi na kutatua changamoto mbalimbali.

**67.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango inakadiriwa kukusanya **TZS 2.49 trilioni.** Makadirio hayo ni ongezeko la asilimia 28 ikilinganishwa na makadirio ya kukusanya TZS 1.783 trilioni yaliyopangwa mwaka 2021/2022.

**68.** **Mheshimiwa Spika,** Mapato hayo yamekadiriwa kukusanywa katika mafungu ya Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango kama ifuatavyo:
i. Fungu F01 limekadiriwa kukusanya TZS 1.79 trilioni;
ii. Fungu F04 limekadiriwa kukusanya TZS 185 milioni; na
iii. Fungu F05 limekadiriwa kukusanya TZS 698 bilioni.

Mchanganuo wa Mapato yanaonekana katika **kiambatisho Namba. 4**

## Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Rais- Fedha na Mipango

69. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa Fedha 2022/2023, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango inakadiriwa kutumia TZS 653.07 bilioni kwa mafungu sita (6) yenye programu kuu kumi na tatu(13) na programu ndogo arubaini (40) yanayosimamiwa na Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango. Uchambuzi wa matumizi yake ni kama ifuatavyo:
    i. Fungu F01 limekadiriwa kutumia TZS 394.37 bilioni;
    ii. Fungu F02 limekadiriwa kutumia TZS 211.60 bilioni;
    iii. Fungu F03 limekadiriwa kutumia TZS 18.93 bilioni;
    iv. Fungu F04 limekadiriwa kutumia TZS 17.05 bilioni;
    v. Fungu F05 limekadiriwa kutumia TZS 7.49 bilioni; na
    vi. Fungu F06 limekadiriwa kutumia TZS 3.63 bilioni.

70. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 matumizi ya Fungu F01 yamekadiriwa kufikia jumla ya TZS 394.37 bilioni. Mchanganuo wa matumizi hayo kiprogramu ni kama ifuatavyo:

**PF0101- Programu Kuu ya Usimamizi wa Bajeti na Fedha za Umma**

71. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inaombewa kuidhinishiwa matumizi ya TZS 227.49 bilioni kwa kutekeleza programu ndogo nne (4) zifuatazo:
**SF010102**-Usimamizi wa Bajeti ya Serikali TZS 172.27 bilioni;
**SF010103-** Uratibu wa Rasilimali za Nje TZS 430.89 milioni;
**SF010105-** Usimamizi wa Sekta ya Fedha na Sera za Kodi TZS 53.82 bilioni; na
**SF010106-** Usimamizi wa Mifumo ya Udhibiti wa Fedha za Umma TZS 963.21 millioni.

**PF0102 – Programu ya Usimamizi na Uwekezaji wa Mali za Umma**

72. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inaombewa kuidhinishiwa matumizi ya TZS 107.52 bilioni kwa kutekeleza programu ndogo mbili (2) zifuatazo:
**SF010201-** Usimamizi wa Mitaji ya Umma TZS 106.78 bilioni; na
**SF010202-** Usimamizi wa Ununuzi na Uhakiki wa Mali za Serikali TZS 745.13 milioni.

**PF010104- Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango**

73. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inaombewa kuidhinishiwa matumizi ya TZS 59.34 bilioni kwa kutekeleza programu ndogo tatu (3) zifuatazo:
**SF010401-** Utawala na Uendeshaji wa Ofisi TZS 4.32 bilioni;
**SF010402-** Mipango, Sera na Utafiti wa Sekta ya Fedha TZS 51.79 bilioni; na
**SF010403-** Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Ofisi-Pemba-TZS 3.22 bilioni.

74. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Matumizi ya Fungu F02 yamekadiriwa kufikia jumla ya TZS 211.60 bilioni. Mchanganuo wa matumizi hayo kiprogramu ni kama ifuatavyo:

**PF0201 – Programu Kuu ya Usimamizi wa Mfuko Mkuu wa Serikali**

75. **Mheshimiwa Spika**, Programu hii inaombewa kuidhinishiwa matumizi ya TZS 211.60 bilioni kwa kutekeleza program ndogo moja (1) ifuatayo:
**SFO2O101 –** Usimamizi wa Mfuko Mkuu wa Serikali TZS 211.60 bilioni.

76. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Matumizi ya Fungu F03 (Tume ya Mipango) yamekadiriwa kufikia jumla ya TZS 18.93 bilioni. Mchanganuo wa matumizi hayo kiprogramu ni kama ifuatavyo:

**PF0301 - Programu Kuu ya Uratibu wa Mipango ya Kitaifa na Maendeleo ya Watendakazi**

77. **Mheshimiwa Spik**a, Programu hii inaombewa kuidhinishiwa matumizi ya jumla ya TZS 14.92 bilioni kwa kutekeleza programu ndogo tatu (3) zifuatazo:
**SF030101**–Uratibu wa Mipango ya Kitaifa na Kupunguza Umaskini TZS 12.87 bilioni;
**SF030102**– Maendeleo ya Watendakazi na Masuala ya Idadi ya Watu TZS 901.35 milioni; na
**SF030103**–Ufuatiliaji na Tathmini wa Mpango wa Maendeleo TZS 1.15 bilioni.

**PF0302 - Programu Kuu ya Usimamizi wa Uchumi Mkuu na Utafiti**

78. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inaombewa kuidhinishiwa matumizi ya TZS 1.51 bilioni kwa kutekeleza programu ndogo mbili (2) zifuatazo:
**SF030201**-Ukuzaji wa Uchumi TZS 579.39 milioni; na
**SF030202**- Uratibu wa Tafiti na Ubunifu TZS 933.92 milioni.

**PF0303 - Programu Kuu ya Uendeshaji na Utumishi wa Tume ya Mipango**

79. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inaombewa kuidhinishiwa matumizi ya jumla ya TZS 2.49 bilioni kwa kutekeleza programu ndogo mbili (2) zifuatazo:
**SF030301**-Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Mipango Unguja TZS 2.01 bilioni; na

**SF030302**-Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Tume ya Mipango Pemba TZS 484.30 milioni.

**80.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Matumizi ya Fungu F04 (Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali) yamekadiriwa kufikia jumla ya TZS 17.05 bilioni. Mchanganuo wa matumizi hayo kiprogramu ni kama ifuatavyo:

**PF0401- Programu Kuu ya Kuendeleza na Kuratibu Takwimu rasmi za Kiuchumi na Kijamii**

**81.** **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inaombewa kuidhinishiwa matumizi ya jumla ya TZS 12.73 bilioni kwa kutekeleza programu ndogo mbili (2) zifuatazo:
**SF040101**-Ukusanyaji, Uchambuzi na Uwasilishaji wa Takwimu rasmi za Kiuchumi na Kijamii TZS 10.86 bilioni; na
**SF040102**-Uratibu wa Shughuli za Takwimu katika Mfumo wa Taifa wa Takwimu Zanzibar TZS 1.87 bilioni.

**PF0402- Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali**

**82.** **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inaombewa kuidhinishiwa matumizi ya TZS 4.28 bilioni kwa kutekeleza programu ndogo mbili (2) zifuatazo:
**SF040201-**Utawala na Uendeshaji Unguja TZS 3.76 bilioni; na
**SF040202-** Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Takwimu Pemba TZS 512.83 milioni.

**83.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Matumizi ya Fungu F05 (Mhasibu Mkuu wa Serikali) yamekadiriwa kufikia jumla ya TZS 7.48 bilioni. Mchanganuo wa matumizi hayo kiprogramu ni kama ifuatavyo:

**PF0501- Programu Kuu ya Usimamizi wa Hazina**

**84. Mheshimiwa Spika,** Programu hii inaombewa kuidhinishiwa matumizi ya TZS 899.46 milioni kwa kutekeleza programu ndogo tatu (3) zifuatazo:

**SF050101**-Ufuatiliaji wa Mapato ya Serikali Yasiyokua ya Kodi TZS 108.97 milioni;

**SF050102**-Kusimamia Ufungaji wa Hesabu Jumuishi za Serikali TZS 220.12 milioni; na

**SF050102-**Usimamizi wa Matumizi ya Serikali TZS 570.37 milioni.

**PF0502- Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Mhasibu Mkuu**

**85. Mheshimiwa Spika,** Programu hii inaombewa kuidhinishiwa matumizi ya TZS 6.58 bilioni kwa kutekeleza programu ndogo mbili (2) zifuatazo:

**SF050201**-Utawala na Uendeshaji Unguja TZS 5.32 bilioni; na

**SF050202**-Utawala na Uendeshaji Pemba TZS 1.25 bilioni.

**86. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Matumizi ya Fungu F06 (Ukaguzi wa Ndani) yamekadiriwa kufikia jumla ya TZS 3.63 bilioni. Mchanganuo wa matumizi hayo kiprogramu ni kama ifuatavyo:

**PF0601- Programu Kuu ya Usimamizi wa Ukaguzi wa Ndani Serikalini**

**87. Mheshimiwa Spika,** Programu hii inaombewa kuidhinishiwa matumizi ya TZS 1.13 bilioni kwa kutekeleza program ndogo tatu (3) zifuatazo:

**SF060101**-Usimamizi wa Kamati za Ukaguzi na Taarifa TZS 307.50 milioni;

**SF060102**-Uchunguzi wa Ubadhirifu na Vihatarishi TZS 696.43 milioni; na

**SF060103**-Usimamizi wa Uthibitisho wa Ubora TZS 134.54 milioni.

**PF0602 - Programu Kuu ya Utawala na Uendeshaji**

88. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inaombewa kuidhinishiwa matumizi ya TZS 2.49 bilioni kwa kutekeleza program ndogo mbili (2) zifuatazo:
**SF060201**-Usimamizi wa Rasilimali Watu, Mipango, Matumizi, Mafunzo na Utafiti TZS 1.87 bilioni; na
**SF060202**-Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Ofisi Pemba TZS 623.17 milioni.

## K. MIRADI YA MAENDELEO ITAKAYOSIMAMIWA NA OFISI YA RAIS - FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA 2022/2023

89. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Miradi, Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango inatarajia kusimamia na kutekeleza miradi tisa (9) ya maendeleo katika mwaka wa fedha 2022/2023 kama ifuatavyo:

### i. Mradi wa Ushajihishaji Upatikanaji Rasilimali Fedha (ISP-DRMNRG)

90. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Mradi huu unakadiriwa kutumia TZS 1.46 bilioni chini ya ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) Mradi huu unalenga kushajiisha utafutaji wa rasilimali fedha ndani na nje ya Nchi.

### ii. Mradi wa Ukuzaji Uchumi Jumuishi Zanzibar (BIG-Z)

91. **Mheshimkwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, mradi huu unakadiriwa kutumia TZS 47.13 bilioni chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia (WB) Mradi huu unalenga kuimarisha hali ya maisha na kukuza maendeleo ya Kiuchumi katika Maeneo ya Unguja na Pemba.

**iii. Mradi wa Mageuzi ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP)**

92. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Mradi huu unakadiriwa kutumia TZS 2.66 bilioni chini ya ufadhili wa *Norway* Mradi huu unalenga kuleta Mageuzi katika Usimamizi wa Fedha za Umma.

**iv. Mradi wa Ujenzi wa Ofisi za Serikali**

93. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, mradi huu unakadiriwa kutumia TZS 92.20 bilioni kwa Lengo la kuimarisha ufanisi wa utendaji Serikalini kwa kutengeneza Ofisi mbali mbali.

**v. Kuratibu Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)**

94. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, mradi huu unakadiriwa kutumia TZS 4.50 bilioni. Programu hii inalenga kuwakwamua wananchi na umasikini kupitia urasimishaji wa biashara na ardhi ili iweze kutumika katika kujiletea maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

**vi. Mradi wa Kupunguza Umasikini na Ukuaji wa Uchumi**

95. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, mradi huu unakadiriwa kutumia TZS 800.00 milioni. Mradi huu unalenga kufanya tafiti ndogo ndogo kwa Shehia zilizoripotiwa kuwa na umasikini kutokana na Ripoti ya Matumizi ya Kaya (HBS) kwa lengo la kuja na mbinu mbali mbali ikiwemo miradi midogo ya wananchi ya kupunguza umasikini.

**vii. Mradi wa Usimamizi wa Upembuzi yakinifu wa Programu na Miradi ya Maendeleo.**

96. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, mradi huu unakadiriwa kutumia TZS 6.98 bilioni. Mradi huu unalenga kufanya uratibu na usimamizi wa uandaaji wa upembuzi yakinifu na mapitio ya Sekta za kijamii na kiuchumi (sector review).

**viii. Mradi wa Usimamizi, Kujenga Uwezo na Kuoanisha Mipango ya Kisekta, Kitaifa na Kimataifa**

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, mradi huu umepangiwa kutumia TZS 530 milioni chini ya ufadhili wa UNDP na SMZ kwa lengo la kuimarisha usimamizi na kuoanisha Mipango ya Kisekta, Kitaifa, Kikanda na Kimataifa ikiwemo Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP), Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) na Malengo ya Maendeleo ya Africa (Africa Agenda 2063).

**ix. Mradi wa Uendelezaji Takwimu (ZSDP)**

97. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Mradi huu unakadiriwa kutumia TZS 13.26 bilioni chini ya ufadhili wa UNFPA, UNICEF, UN-Women na USAID kwa lengo la kukusanya, kuchambua na kutoa takwimu rasmi za kiuchumi na kijamii. Orodha ya miradi inayosimamiwa na Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango **Kiambatisho Namba 5.**

## L. MWELEKEO WA BAJETI KWA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA OFISI YA RAISI - FEDHA NA MIPANGO 2022/2023

### 1) Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB)

98. **Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Mapato Zanzibar inaendelea na kazi ya uwakala wa Serikali wa kukusanya mapato yatokanayo na vianzio mbali mbali vya kodi. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, ZRB inakadiriwa kukusanya jumla ya TZS 579.50 bilioni kutoka katika

vyanzo vilivyoainishwa katika kitabu cha Mswada wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2022/2023.

99. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Matumizi ya Bodi ya Mapato Zanzibar inakadiriwa kutumia TZS 28.07 bilioni kwa ajili ya kutekeleza shughuli zake za kawaida na maendeleo. Miongoni mwa shughuli hizo ni:

i. Kukusanya Mapato ya Serikali TZS 579.50 bilioni;
ii. Kuendelea na kaguzi katika Hoteli kubwa za Kitalii, Kampuni za Mawasiliano na Taasisi za Fedha;
iii. Kuendelea kusajili walipakodi katika mfumo wa kutolea risiti za kielektroniki (VFMS);
iv. Kuunganisha mfumo wa VFMS na mifumo mengine ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa za kodi;
v. Kuongeza ukusanyaji wa mapato kwa kuimarisha mifumo ya kielektroniki na taratibu za utendaji kazi;
vi. Kuimarisha taratibu za utendaji kazi kwa kutumia mifumo ya kilektroniki;
vii. Kuongeza ubunifu katika Teknolojia ya Habari na mawasiliano (TEHAMA);
viii. Kuendelea kuwatambua na kuwasajili walipakodi wapya wapatao elfu sita (6000). Mkoa wa Mjini Magharibi 3000, Mkoa wa Kaskazini Unguja 1000, Kusini Unguja 1000, Kaskazini Pemba 500 na Kusini Pemba 500.
ix. Kuhamasisha ulipaji kodi wa hiari, kutoa na kudai risiti;
x. Kutoa ajira za muda; na
xi. Kuanzishwa kwa Ofisi za Mikoa.

### 2) Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)

100. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa Tawi la Zanzibar inaendelea na kazi ya uwakala wa Serikali wa kukusanya mapato ya kodi. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, TRA imekadiriwa kukusanya TZS 454.05 bilioni kutoka katika vyanzo vilivyoainishwa

katika kitabu cha Mswada wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2022/2023.

101. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Mapato Tanzania imejipanga kuongeza ukusanyaji wa mapato kwa kuimarisha mifumo ya kielektroniki ifuatayo:

i. Mfumo wa kusajili walipakodi (Online TIN Registration). Kupitia mfumo huu, wafanyakazi na wafanyabiashara wanaweza kujisajili kwa simu za mkononi bila ya ulazima wa kufika katika ofisi za TRA;
ii. Mfumo wa kuwasilisha Ritani (Return Filing System). Kupitia mfumo huu wafanyabiashara wanaweza kuwasilisha ritani zao kwa simu za mkononi ili kurahisisha uwasilishaji wa ritani za kodi;
iii. Mfumo wa 'Government Electronic Payments Gateaway (GePG)' ambapo mlipakodi anaweza kulipa kodi yake akiwa popote kwa kutumia simu ya mkononi;
iv. Mfumo wa 'TANCIS' ambao unasaidia kudhibiti uingizaji na usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi; na
v. Mfumo wa 'Transire Process' ambao unasaidia kudhibiti magendo kwenye biashara ya usafirishaji wa majahazi.

### 3) Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF)

102. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa Fedha 2022/2023, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ZSSF, unatarajia kukusanya TZS 166.4 bilioni kutokana na vyanzo vikuu wiwili ambavyo; ni makusanyo ya michango ya wanachama wa Serikali, Taasisi Binafsi na waliojiajiri wenyewe jumla ya TZS 102.9 bilioni na faida inayotokana na uwekezaji wa muda mrefu na muda mfupi wa masoko ya fedha na mitaji jumla ya TZS 63.5 bilioni.

103. **Mheshimiwa Spika,** Mfuko unategemea kutumia TZS 166.4 bilioni kwa mwaka 2022/2023. Kati ya fedha hizo TZS 10.2 bilioni

zinategemewa kutumika kwa matumizi ya uendeshaji, TZS 58.4 bilioni kwa kulipia mafao ya wanachama na TZS 97.8 bilioni kwa ajili ya uwekezaji.

104. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, ZSSF imepanga kuanzisha Ujenzi wa nyumba za bei nafuu katika maeneo tofauti kwa kushirikiana na Serikali kulingana na upatikanaji wa ardhi. Kwa upande wa mradi wa nyumba za bei nafuu za Mombasa, tayari Mfuko umekamilisha taratibu za kumpata Mshauri Elekezi na unaendelea na hatua za kusaini mikataba na hatimae kuandaa vitabu vya zabuni.

105. **Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa hifadhi ya jamii umepanga kutekeleza yafuatayo:

i. Kuendelea kufungua Ofisi za kutoa huduma za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar katika Mikoa ya Unguja na Pemba ikiwa ni moja ya utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020-2025;

ii. Kuangalia utaratibu wa kuanzisha dirisha la utoaji wa huduma ya Hifadhi ya Jamii na uwekezaji kwa kutumia sharia na miongozo ya Kiislam (Islamic Social Security) pamoja na Idara ya Usimamizi na Udhibiti (Support and Control). Kazi hii ipo katika hatua za kutafuta mshauri elekezi;

iii. Kufanya utafiti kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali (OCGS) wenye lengo la kuongeza wigo wa wanachama hadi kufikia asilimia 50 ikiwa pia ni utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020-2025;

iv. Kuendeleza mashirikiano kwa taasisi za Serikali kwa lengo la kuimarisha usajili wa wanachama na kuwasilisha michango na pia kusaidia ukusanyaji wa mapato ya Serikali;na

v. Kufanya tathmini ya uhai wa mfuko kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

106. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa miradi, ZSSF kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imepanga kutekeleza Miradi ifuatayo:

i. Kukamilisha awamu ya pili ya mradi wa Mbweni (Mpya na Kongwe), ambayo ipo katika hatua za manunuzi za kumtafuta mashauri elekezi;
ii. Kutekeleza Mradi wa eneo la maegesho ya magari Michenzani, ambalo tayari Mkandarasi ameshasaini mkataba wa ujenzi;
iii. Kushirikiana na Umoja wa Watu wenye Ulemavu katika Mradi wa Makaazi Mombasa kama inavyoonyeshwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020-2025 ambayo ipo katika hatua ya Manunuzi ya kumtafuta Mshauri elekezi;
iv. Ujenzi wa vituo vya Daladala na jengo la kuegesha gari katika eneo la Kijangwani na Malindi;
v. Ujenzi wa Soko la Mombasa; na
vi. Kuendelea kuwekeza fedha kwa kipindi cha muda mfupi na muda mrefu katika hatifungani, hatifungati, uwekezaji katika mabenki na kuendelea kutoa mikopo yenye tija kwa Serikali, Mashirika, Taasisi na Kampuni Binafsi.

### 4) Mfuko wa Barabara (ZRF)

107. **Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Barabara Zanzibar unaendelea na jukumu la kudumisha utunzaji wa fedha zinazokusanywa kwa ajili ya matengenezo ya barabara kwa dhamira ya kuwa na miundombinu endelevu. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Mfuko unatarajiwa kutumia TZS 22.17 bilioni kwa kazi zifuatazo:

i. Kukamilisha matengenezo ya barabara TZS 20.03 bilioni;
ii. Ujenzi wa madaraja-Unguja: Daraja la Machui, Daraja la Mtopepo na Daraja la Pangatupu na kwa upande wa Pemba: Daraja la Vitongoji, Daraja la Chamanangwe na Daraja la Pondeani.
iii. Matengenezo ya muda maalum barabara za kifusi

**108. Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Unguja ni kukamilisha matengenezo ya barabara zifuatazo:

i. Kuendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa barabara ya Jozani – Charawe – Ukongoroni – Bwejuu (23.2km);
ii. Barabara ya Unguja Ukuu – Uzi- Ng'ambwa (7km);
iii. Barabara ya Tumbatu (9 km);
iv. Barabara ya Garagara – Chemchem – Mtoni Kidatu (3km);
v. Barabara ya Kiboje – Uchukuchuni (3.1 km); na
vi. Barabara ya Kizimbani – Kiboje 7.2 km.

**109. Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Pemba ni kukamilisha matengenezo ya barabara zifuatazo:

i. Kuendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa barabarara ya Kipapo – Mgelema – Wambaa kwa kiwango cha lami (9.3 km);
ii. Uwekaji wa lami barabara ya Kijangwani – Birikau ( 4.2 km); na
iii. Barabara ya Micheweni Msituni – Mjini Wingwi – Msasani kwa kiwango cha lami (3.5 km).
iv. Matengenezo ya kawaida barabara za lami.

**110. Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Barabara utatengeneza barabara zifuatao zilizojengwa kwa lami baridi za Mradi wa 'PRRP' :

i. Chanjamjawiri-Tundauwa (11km);
ii. Chanjaani-Pujini (5km);
iii. Mzingani-Wambaa (5km);
iv. Kenya-Chambani (3.2km);
v. Mtambile-Kangani (6.4km); na
vi. Mtambile-Kengeja (9.6km.).

### 5) Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma (ZPPDA)

**111. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za umma, Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, imekadiriwa kukusanya

TZS 300 milioni kutoka katika vyanzo vyake vya mapato na inaombewa kuidhinishwa matumizi ya TZS 2.273 bilioni ambayo ni ruzuku kutoka Serikalini. Mamlaka itaendelea kutekeleza majukumu yake ya kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Namba 11 ya Mwaka 2016 kwa lengo la kuhakikisha taratibu za kisheria zinafuatwa na thamani halisi ya fedha katika manunuzi inakuwepo.

### 6) Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ)

112. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Benki ya PBZ inatarajia kukusanya mapato jumla ya TZS 114.53 bilioni na matumizi ya TZS 78.99 bilioni yanatarajiwa kutumika kwa mwaka 2022 kwa ajili ya riba na matumizi yasio ya riba. Rasilimali za benki zinatarajiwa kukua kutoka TZS 996.00 billioni hadi TZS 1,159.00 bilioni. Ukuwaji huu unatarajiwa kuchangiwa na ongezeko la mikopo kwa wateja kutoka TZS 602.00 bilioni hadi kufikia TZS 732.00 bilioni;

113. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa amana za wateja Benki inatarajia kuongeza amana zake kutoka kwa wateja wake hadi kufikia TZS 917.00 bilioni kutoka TZS 758.00 bilioni. Aidha, mtaji unatarajiwa kukua kwa asilimia 16 kutoka TZS 122.00 bilioni hadi TZS 146.00 bilioni. Benki inatarajia vile vile kupata faida ya TZS 35.54 bilioni kwa mwaka 2022 kulinganisha na faida ya mwaka 2021 iliyopatikana TZS 22.69 bilioni ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 57.

114. **Mheshimiwa Spika,** PBZ itajikita zaidi katika kutekeleza mambo makuu yafuatayo:

i. Kuanzisha bidhaa na huduma mpya za benki ya kiislamu zitakazovutia zaidi wateja;
ii. Kufanya upembuzi yakinifu katika mikoa ya Mwanza, Arusha, Mbeya, Morogoro na Tanga ili kuweza kufungua

huduma za kibenki katika maeneo hayo;

iii. Kuimarisha huduma za mawakala ili kuondoa tatizo la foleni kwenye matawi yake, pamoja na maeneo ya kambi za jeshi kwa kuongeza vituo vya kutoa huduma (POS) 1000 kila mwaka;

iv. Kuanzisha kituo maalum cha huduma kwa wateja kitakachofanya kazi saa 24 ili kuweza kupokea na kufanyia kazi changamoto za wateja wetu kwa wakati na haraka;

v. Kufungua vituo vya kutolea huduma katika maeneo ya Konde, Kinyasini, Tunguu, Dunga, Nungwi, Mbagala na Masasi Mtwara;

vi. Kufungua vituo vya kubadilisha fedha, (Bureau De Change) katika maeneo ya Paje, Michamvi, Marumbi na Uwanja wa ndege Dar es Salaam; na

vii. Kuweka mashine 11 za kutolea fedha katika maeneo ya Gombani, Konde, Mtambile, Amani, Maungani na Kinyasini, Mpendae na Bavuai.

### 7) Shirika la Bima la Zanzibar (ZIC)

**115. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Shirika la Bima Zanzibar linatarajia kukusanya TZS 46.8 bilioni kutoka katika vianzio vyake vya mapato ya biashara ya bima na uwekezaji kwa kutekeleza mikakati ifuatayo:

i. Kuanzisha Kampuni Tanzu itakayosimamia Uendeshaji wa Bima ya Kiislam 'TAKAFUL' kwa lengo la kuongeza mapato ya Shirika na kurahisisha miamala ya kiuchumi ndani ya nchi;

ii. Kuanzisha aina mpya ya kinga za Bima ya Maisha 'LIFE ASSURANCE' na kinga za Bima ya Wasafiri (TRAVEL INSURANCE) kwa lengo la kuongeza mapato ya Shirika na kutanua wigo wa biashara ya bima Tanzania;

iii. Kuendelea kutekeleza kauli mbiu ya Serikali katika kutoa kinga za bima katika maeneo yote yanayohusiana na uchumi wa buluu Zanzibar na Tanzania;

iv. Kufanya upembuzi yakinifu wa kuweza kufungua ofisi za mauzo kwa upande wa Tanzania Bara katika maeneo ambayo hakuna ofisi hizo.
v. Kutoa taaluma kwa Wananchi na Taasisi za Serikali na binafsi juu ya suala la kujiwekea kinga mali zao kwa lengo la kuongeza idadi ya wateja wapya na biashara mpya zisizokuwa za magari katika mtandao wake;
vi. Kuzidisha mashirikiano na mawakala na madalali wanaofanya biashara ya kuuza bima kwa niaba ya shirika;
vii. Kushirikiana kikamilifu na mabenki katika mfumo wa 'Bank Assurance' kwa lengo la kuongeza mapato; na
viii. Kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano Tanzania kwa kuhakikisha miradi yote mikubwa ya maendeleo kwa wananchi inakatiwa kinga za Bima na Shirika.

116. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa matumizi, Shirika la Bima kwa mwaka wa fedha 2022/2023 limepanga kutumia jumla ya TZS 10.5 bilioni ikijumuisha matumizi yafuatayo:
i. Matumizi kwa kazi za kawaida za Shirika TZS 9.8 bilioni;
ii. Matumizi ya ununuzi wa vitendea kazi TZS 501 milioni; na
iii. Ununuzi wa magari mawili kwa matumizi ya Shirika TZS 212 milioni.

## M. SHUKRANI

117. **Mheshimiwa Spika,** Matayarisho ya Bajeti yamehusisha wadau wengi, wakiwemo watendaji wa Ofisi yetu na taasisi mbali mbali ambao tumeshirikiana kukamilisha suala hili.

118. **Mheshimiwa Spika,** Naomba kutoa shukrani za dhati kwa Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais- Fedha na Mipango Mheshimiwa Ali Suleiman Mrembo na wafanyakazi wa Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango wakiongozwa na Katibu Mkuu Dkt. Juma Malik Akil, Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango Dkt. Rahma Salum

Mahfoudh, Naibu Katibu Mkuu Fedha na Mipango Nd. Aboud Hassan Mwinyi na Naibu Katibu Mkuu Mifumo Nd. Rashid Said Rashid pamoja na Wakuu wa Taasisi chini ya Wizara kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuhakikisha kuwa majukumu ya wizara yanatekelezwa kwa ufanisi.

**119.** **Mhshimiwa Spika,** Naomba kwa ruhusa yako kuchukua nafasi hii kutoa wito kwa wananchi wote kushiriki katika zoezi la Sensa ya Watu na Makaazi, na kuwa tayari kuhesabiwa ifikapo tarehe 23 Agosti, 2022. Sensa ya Watu na Makaazi ni muhimu sana kwa kuzingatia matokeo ya kazi ya Sensa yatasaidia kuimarisha mipango ya nchi. Aidha, kukabiliana na changamoto mbali mbali zinazohusiana na uchumi na maendeleo.

## N. HITIMISHO

**120.** **Mheshimiwa Spika,** Baada ya maelezo niliyoyatoa, kwa heshima, naomba Baraza lako tukufu kuidhinisha mapendekezo ya ukusanyaji wa mapato ya TZS 2.49 trilioni zitakazokusanywa na Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Aidha, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha matumizi ya TZS 653.07 bilioni kwa mafungu yafuatayo:

i. Fungu F01, naomba kuidhinishiwa TZS 394.37 bilioni;
ii. Fungu F02, naomba kuidhinishiwa TZS 211.60 bilioni;
iii. Fungu F03, naomba kuidhinishiwa TZS 18.93 bilioni;
iv. Fungu F04, naomba kuidhinishiwa TZS 17.05 bilioni;
v. Fungu F05 naomba kuidhinishiwaTZS na TZS 7.49 bilioni; na
vi. Fungu F06 naomba kuidhinishiwa TZS 3.63 bilioni.

**121.** **Mheshimiwa Spika,** naomba Baraza lako tukufu kuidhinisha matumizi ya mafungu hayo ili kuyawezesha kutekeleza shughuli zilizopangwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

122. **Mheshimiwa Spika,** Maelezo na shughuli zitakazotekelezwa kwa mwaka 2022/2023 yanapatikana katika Kitabu cha Nne (Volume IV) cha Mswada wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Bajeti inayotumia PBB.

123. **Mheshimiwa Spika,** Kwa heshima, naomba kutoa hoja.

**MHE. DKT. SAADA MKUYA SALUM,**
**WAZIRI WA NCHI,**
**OFISI YA RAIS-FEDHA NA MIPANGO**

**KIAMBATANISHO NO 1**

**MUHTASARI WA MAPATO KWA KIPINDI CHA JULAI - MACHI, 2022**

| VIANZIO | MAKADIRIO 2021/2022 | MAKADIRIO JULAI - MACHI,2022 | HALISI JULAI - MACHI,2022 | ASILIMIA KWA MWAKA | ASILIMIA KWA MIEZI TISA |
|---|---|---|---|---|---|
| **MAPATO YA KODI** | | | | | |
| MAMLAKA YA MAPATO (TRA) | 413,064,254,000.00 | 256,366,735,225.82 | 256,361,735,225.82 | 62% | 100% |
| BODI YA MAPATO ZANZIBAR (ZRB) | 525,095,093,000.00 | 275,201,115,915.67 | 275,179,115,915.67 | 52% | 100% |
| UHAMISHO WA MAPATO YA WAFANYAKAZI | 21,000,000,000.00 | 15,750,000,000.00 | 11,034,320,152.00 | 53% | 70% |
| **JUMLA NDOGO** | **959,159,347,000.00** | **547,317,851,141.49** | **542,575,171,293.49** | **57%** | **99%** |
| **MIKOPO YA NDANI** | | | | | |
| HATI FUNGANI (T/BOND) | 92,000,000,000.00 | 92,000,000,000.00 | 100,000,000,000.00 | 109% | 109% |
| MIKOPO KWA MIRADI YA MAENDELEO | 220,000,000,000.00 | - | - | 0% | 0% |
| **JUMLA NDOGO** | **312,000,000,000.00** | **92,000,000,000.00** | **100,000,000,000.00** | **32%** | **109%** |
| **FEDHA ZA WASHIRIKA WA MAENDELEO** | | | - | | |
| RUZUKU KUTOKA NJE | 79,070,555,000.00 | 54,211,502,959.00 | 37,027,670,409.88 | 47% | 68% |
| MKOPO KUTOKA WASHIRIKA | 204,025,578,000.00 | 153,019,183,475.00 | 82,472,624,956.48 | 40% | 54% |
| **JUMLA NDOGO** | **283,096,133,000.00** | 207,230,686,434.00 | 119,500,295,366.36 | 42% | 58% |
| MSAADA WA KIBAJETI (GBS) | **20,000,000,000.00** | 5,000,000,000.00 | 2,348,388,513.01 | 12% | 47% |
| **JUMLA NDOGO** | **1,574,255,480,000.00** | **851,548,537,575.49** | **764,423,855,172.86** | **49%** | **90%** |
| **MAPATO YASIYOKUWA YA KODI** | | | | | |
| GAWIO LA MASHIRIKA | 35,750,000,000.00 | 35,750,000,000.00 | 5,803,553,000.00 | 16% | 16% |
| GAWIO KUTOKA BOT | 15,000,000,000.00 | 15,000,000,000.00 | 9,000,000,000.00 | 60% | 60% |
| UHAMIAJI | 64,474,278,000.00 | 52,226,418,393.00 | 37,866,771,688.79 | 59% | 73% |
| MCHANGO MAMLAKA(ZURA) | 6,000,000,000.00 | 4,500,000,000.00 | 4,500,000,000.00 | 75% | 100% |
| KODI YA BOHARI | 1,117,055,000.00 | 855,400,000.00 | 399,037,196.00 | 36% | 47% |
| **JUMLA NDOGO** | **122,341,333,000.00** | **108,331,818,393.00** | **57,569,361,884.79** | **47%** | **53%** |
| **MAPATO MENGINEYO YASIYOKUWA YA KODI** | | | | | |
| MABUKU NA STAKABADHI-UNGUJA | 72,615,000.00 | 55,264,070.00 | 15,625,500.00 | 22% | 28% |
| MABUKU NA STAKABADHI-PEMBA | 11,785,000.00 | 7,950,000.00 | 10,120,000.00 | 86% | 127% |
| USAJILI WA WAZABUNI | 444,419,000.00 | 318,801,000.00 | 144,876,500.00 | 33% | 45% |
| NYARAKA ZA ZABUNI | 8,264,000.00 | 8,264,000.00 | 7,500,000.00 | 91% | 91% |
| KODI YA NYUMBA ZA SERIKALI | 1,123,618,000.00 | 557,698,000.00 | 37,312,300.00 | 3% | 7% |
| VIFAA VIKONGWE-UNGUJA | 480,456,000.00 | 388,945,000.00 | 757,865,400.00 | 158% | 195% |
| VIFAA VIKONGWE-PEMBA | 141,122,000.00 | 108,450,000.00 | 132,304,700.00 | 94% | 122% |
| ADA YA UKODISHWAJI UKUMBI-PEMBA | 12,175,000.00 | 9,300,000.00 | 7,740,000.00 | 64% | 83% |
| MCHANGO KUTOKA BODI YA WASANIFU | 564,483,000.00 | 442,085,000.00 | 270,930,569.51 | 48% | 61% |
| MCHANGO KUTOKA BODI YA WAKANDARASI | 1,355,192,000.00 | 922,965,375.00 | 401,625,509.93 | 30% | 44% |
| MCHANGO KUTOKA BODI YA UHAULISHAJI ARD | 3,131,297,000.00 | 2,350,849,500.00 | 1,399,749,754.00 | 45% | 60% |
| MAUZO YA MADINI | - | - | 11,111,100,000.00 | 0% | 0% |
| BAKAA LA MWAKA ULIOPITA | 80,000,000,000.00 | 80,000,000,000.00 | | 0% | 0% |
| **JUMLA NDOGO** | **87,345,426,000.00** | **85,170,571,945.00** | **14,296,750,233.44** | **16%** | **17%** |
| **JUMLA KUU** | **1,783,942,239,000.00** | **1,045,050,927,913.49** | **836,289,967,291.09** | **47%** | **80%** |
| **Chanzo OR -Fedha na Mipango** | | | | | |

KIAMBATANISHO NO 2

**MATUMIZI YA OFISI YA RAIS, FEDHA NA MIPANGO JULAI - MACHI, 2022**

Tarakimu ni milioni

| Programu Kuu | Programu ndogo | Makisio Mwaka Julai-Juni ( 2021-2022) | Makisio Julai - Machi 2022 | Mishahara | Matumizi ya Mengineyo | Maendeleo | | Ruzuku | Jumla | Asilimia ya Fedha zilizopatikana kwa Miezi Tisa | Asilimia ya Fedha zilizopatikana kwa Mwaka |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | SMZ | Mhisani | | | | |
| Usimamizi wa bajeti na Fedha za Umma | Usimamizi wa hazina | 35,012.85 | 24,890.58 | 2,921.54 | 371.95 | | | 16,676.56 | 19,970.05 | 80% | 57% |
| | Bajeti | 23,104.30 | 11,844.11 | 269.34 | 10,175.96 | | - | | 10,445.30 | 88% | 45% |
| | Salary Adjustment | | | | | | | | | | |
| | Fedha za Nje | 511.24 | 395.24 | 119.14 | 76.31 | | - | | 195.45 | 49% | 38% |
| | Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Ndani | 1,993.87 | 2,054.10 | 1,269.19 | 297.36 | | | | 1,566.55 | 76% | 79% |
| | Fedha na Sera za Kodi | 1,554.02 | 768.76 | 176.33 | 76.62 | | | | 252.95 | 33% | 16% |
| | Usimamizi wa mifumo ya udhibiti na usimamizi wa fedha za umma | 2,878.91 | 1,280.06 | | 363.98 | | | | 363.98 | 28% | 13% |
| | **Jumla ndogo** | **65,055.19** | **41,232.85** | **4,755.54** | **11,362.18** | **-** | **-** | **16,676.56** | **32,794.28** | 80% | 50% |
| Usimamizi na Uwekezaji wa Mali za Umma | Mitaji ya Umma | 83,592.83 | 40,733.54 | 302.56 | | 34,129.62 | | 761.66 | 35,256.88 | 87% | 42% |
| | Usimamizi wa ununuzi na Uhakiki wa Mali za Serikali | 216.55 | 72.18 | - | 63.04 | | . | | 63.04 | 87% | 29% |
| | **Jumla ndogo** | **83,809.38** | **40,805.72** | **302.56** | **63.04** | **34,129.62** | **-** | **761.66** | **35,319.92** | 87% | 42% |
| Uendeshaji na uratibu wa wizara ya Fedha na Mipango | Utumishi na Uendeshaji | 5,415.63 | 4,170.09 | 822.53 | 2,417.20 | | | - | 3,239.73 | 78% | 60% |
| | Mipango, Sera na Utafiti | 12,331.52 | 7,542.46 | 113.67 | 124.49 | - | 6,014.47 | - | 6,252.63 | 83% | 51% |
| | Ofisi kuu Pemba | 3,396.84 | 3,373.83 | 1,381.90 | 490.00 | | | | 1,871.90 | 55% | 55% |
| | **Jumla ndogo** | **21,143.99** | **15,086.38** | **2,318.10** | **3,031.69** | | **6,014.47** | | **11,364.26** | 75% | 54% |
| | **Jumla F01** | **170,008.56** | **97,124.95** | **7,376.20** | **14,456.91** | **34,129.62** | **6,014.47** | **17,438.22** | **79,478.46** | 82% | 47% |
| Usimamizi wa Mfuko Mkuu wa Serikali | **Usimamizi wa Mfuko Mkuu wa Serikali** | 200,088.80 | 139,284.28 | | 136,950.30 | | | | **132,220.41** | 95% | 66% |
| | **Jumla ndogo** | **208,988.80** | **139,284.28** | | **136,950.30** | | | | **136,950.30** | 98% | 66% |
| | **Jumla F02** | **208,988.80** | **139,284.28** | | **136,950.30** | | | | **136,950.30** | 98% | 66% |
| Kuratibu Mipango ya Kitaifa na Maendeleo ya watendakazi | Uratibu wa Maendeleo ya Kisekta na Kupunguza Umaskini | 3,054.13 | 2,440.24 | 149.43 | 81.44 | 909.44 | 488.93 | | 1,629.24 | 67% | 53% |
| | Maendeleo ya Watendakazi wa Masuala ya Idadi ya Watu | 702.23 | 612.90 | 106.11 | 496.12 | | | | 602.23 | 98% | 86% |
| | Tathmini na Ufuatiliaji wa Mipango ya Maendeleo | 1,094.17 | 940.20 | 195.55 | 190.27 | | 228.65 | | 614.47 | 65% | 56% |
| | **Jumla ndogo** | **4,850.53** | **3,993.34** | **451.09** | **767.83** | **909.44** | **717.58** | **-** | **2,845.94** | 71% | 59% |
| Usimamizi wa Uchumi Mkuu Tafiti na Takwimu | Usimamizi wa Uchumi | 744.24 | 595.21 | 124.06 | 37.84 | | | | 161.90 | 27% | 22% |
| | Kuratibu na kusimamia shughuli za Takwimu Zanzibar | 12,777.26 | 7,995.38 | | | 1,304.11 | 120.00 | 3,172.13 | 4,596.24 | 57% | 36% |
| | Uratibu wa Tafiti na ubunifu | 1,061.42 | 925.45 | 86.36 | 39.14 | | | | 125.50 | 14% | 12% |
| | **Jumla ndogo** | **14,582.92** | **9,516.04** | **210.42** | **76.98** | | **120.00** | **3,172.13** | **4,883.64** | 51% | 33% |
| Uendeshaji na uratibu wa Tume ya Mipango | Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Mipango | 3,182.66 | 2,591.95 | 263.71 | 370.92 | | | | 634.63 | 24% | 20% |
| | Uratibu na Utekelezaji wa shughulu za Tume ya Mipango Pemba | 538.29 | 428.41 | 156.06 | 115.00 | | | | 271.06 | 63% | 50% |
| | **Jumla ndogo** | **3,720.95** | **3,020.36** | **419.77** | **485.92** | | | | **905.69** | 30% | 24% |
| | **Jumla F03** | **23,154.40** | **16,529.74** | **1,081.28** | **1,330.73** | **909.44** | **837.58** | **3,172.13** | **8,635.27** | 52% | 37% |
| | **Jumla F01+F02+F03** | **402,151.76** | **252,938.97** | **8,457.48** | **152,737.94** | **35,039.06** | **6,852.05** | **20,610.35** | **225,064.03** | **89%** | **56%** |

Chanzo OR -Fedha na Mipango

**KIAMBATANISHO NO 3**

**UTEKELEZAJI WA MIRADI INAYOSIMAMIWA NA OFISI YA RAIS FEDHA NA MIPANGO KWA KIPINDI CHA JULAI 2021 HADI MACHI 2022**

| S/N | JINA LA MRADI | MISAADA | MIKOPO | Tarakimu 000 TZS MAKADIRIO | HALISI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Ujenzi wa Ofisi za Serikali | SMZ | | 76,400 | 2,400 |
| 2 | Ukuzaji wa uchumi jumuishi Zanzibar (BIG-Z) | | WORLD BANK | 5,700 | 17,700 |
| 3 | Mradi wa Mageuzi ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP). | NORWAY | | 1,640 | 468.69 |
| 4 | Kuratibu Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) | SMZ | | 2,000 | 1,01 |
| 5 | Mradi wa Uendelezaji Takwimu (ZSDP) | AFDB, USAID, EU, UN Women, GF/UNFPA and BUSKET FUND | | 9,150 | 3,200 |
| 6 | Mradi wa Uimarishaji Rasilimali za Ndani na Usimamizi wa Maliasili (ISP-DRMNRG) | | AFDB | 3,880 | 539.22 |
| 7 | Mradi wa Uimarishaji Utawala Bora (ISPGG III) | | AFDB | 1,506 | 1,502 |

**Chanzo OR - Fedha na Mipango**

KIAMBATANISHO NO 4

## MUHTASARI WA MAPATO YA OFISI YA RAIS, FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

| MAELEZO | MAKADIRIO 2021/2022 (A) | MAKADIRIO 2022/2023 (B) | TOFAUTI |
|---|---|---|---|
| BODI YA MAPATO ZANZIBAR (ZRB) | 525,095,093,000 | 579,502,182,300 | 54,407,089,300 |
| MAMLAKA YA MAPATO (TRA) | 413,064,254,000 | 454,056,838,866 | 40,992,584,866 |
| **JUMLA NDOGO** | **938,159,347,000** | **1,033,559,021,166** | **95,399,674,166** |
| UHAMISHO WA MAPATO YA WAFANYAKAZI | 21,000,000,000 | 14,000,000,000 | - 7,000,000,000 |
| MIKOPO YA NDANI (HATI FUNGANI) | 92,000,000,000 | 115,000,000,000 | 23,000,000,000 |
| MIKOPO KWA MIRADI YA MAENDELEO | 220,000,000,000 | 400,000,000,000 | 180,000,000,000 |
| MIKOPO NA MISAADA KUTOKA KWA ODA | 283,100,000,000 | 673,594,847,000 | 390,494,847,000 |
| GBS | 20,000,000,000 | 10,000,000,000 | - 10,000,000,000 |
| BUSKET FUND | - | 4,370,000,000 | 4,370,000,000 |
| **JUMLA NDOGO** | **636,100,000,000** | **1,216,964,847,000** | **580,864,847,000** |
| **MAPATO YASIO KUWA YA KODI** | | | |
| GAWIO LA MASHIRIKA | 35,750,000,000 | 20,000,000,000 | - 15,750,000,000 |
| KODI YA BOHARI | 1,117,055,000 | 1,065,398,956 | - 51,656,044 |
| MCHANGO MAMLAKA(ZURA) | 6,000,000,000 | 6,000,000,000 | - |
| UHAMIAJI | 64,474,278,000 | 56,597,600,000 | - 7,876,678,000 |
| GAWIO KUTOKA BOT | 15,000,000,000 | 12,000,000,000 | - 3,000,000,000 |
| MAPATO YA UTAFITI | - | 185,000,000 | 185,000,000 |
| **JUMLA NDOGO** | **122,341,333,000** | **95,847,998,956** | **- 26,493,334,044** |
| **MAPATO MENGINEYO YASIYOKUWA YA KODI** | 87,350,000,000 | 144,639,602,000.0 | 57,289,602,000 |
| **JUMLA NDOGO** | **87,350,000,000** | **144,639,602,000** | **57,289,602,000** |
| **JUMLA KUU** | **1,783,950,680,000** | **2,491,011,469,122** | **707,060,789,122** |

**Chanzo OR- Fedha na Mipango**

**KIAMBATANISHO NO. 5**

## MIRADI INAYOSIMAMIWA NA OFISI YA RAIS FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

| S/N | JINA LA MRADI | MISAADA | MKOPO | GHARAMA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Ujenzi wa Ofisi za Serikali | SMZ | | 92,200,000,000 |
| 2 | Ukuzaji wa uchumi jumuishi Zanzibar (BIG-Z) | | WORLD BANK | 47,131,600,000 |
| 3 | Mradi wa Uimarishaji Rasilimali za Ndani na Usimamizi wa Maliasili (ISP-DRMNRG) | | AFDB | 1,460,358,000 |
| 4 | Mradi wa Mageuzi ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP). | | NORWAY | 1,497,280,000 |
| 5 | Kuratibu Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) | SMZ | URT | 4,500,000,000 |
| 6 | Kupunguza umasikini kwa ukuaji wa uchumi | SMZ | | 800,000,000 |
| 7 | Mradi wa Usimamizi wa Upembuzi yakinifu wa Program na Miradi ya Maendeleo | SMZ | | 6,988,539,000 |
| 8 | Mradi wa Kupunguza Umaskini na Ufuatiliaji wa SDGs | SMZ | UNDP | 530,000,000 |
| 9 | Mradi wa Uendelezaji Takwimu (ZSDP) | | UNFPA, UNICEF, UN Women na USAID | 13,200,000,000 |
| | **Jumla Kuu** | | | **168,307,777,000** |
| | **Chanzo OR- Fedha na Mipango** | | | |